Kuvamiwa Kwa Marekani

. . .mapenzi ya Bwana kwa mambo fulani kutukia wakati mwingine. Tulienda Denver, hivi majuzi tu, kisha tukarudi. Ninaamini wao wanataka ripoti, ule mkutano. Ulikuwa mmoja wa mikutano mizuri sana niliyokuwa nayo kwa miaka kadha. Tulikuwa na wakati mzuri sana. Kitu kama zaidi kidogo ya watu elfu mbili walitoa mioyo yao kwa Kristo, mbali na wale walioupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, mbali na ishara kuu na maajabu ambayo Bwana wetu mpendwa Yesu alifanya kati ya watu kule Denver. Wao walipata kumwagwa kwa ajabu, na mkutano mkuu wa watu. Tulianzia na kama watu elfu tano, kwanza. Nasi tulikuwa kwenye Mommoth Gardens. Na kwenye usiku wa tatu, hakukuweko na hata nafasi yo yote ya watu kusimama mahali pale. Tulikuwa na wakati mzuri sana, wa hizo siku tano usiku!

2 Tuliondoka kule, kwenda Canada, mimi pamoja na mvulana wangu. Nasi tukapanda milima, ndipo ikaja mvua ya theluji. Nadhani mmesikia habari zake, kwenye redio zenu. Na watu mia moja themanini na wanane waliangamia kwake. Nasi tulikwama kwenye chungu ya theluji kubwa na upepo kwa—kwa muda wa siku nyingi, kule juu milimani. Ndipo mkutano wetu ukapita, nasi ilitubidi kurudi nyumbani sasa kabla hatujaondoka tena. Kwa hiyo tunaamini yote hayo yalikuwa labda ni mapenzi ya Mungu, kwamba utakuwa mkutano mzuri zaidi, na jambo lingine. Yeye alikuwa ametuandalia kitu fulani ambacho hatujui.

3 Tunatembea kwa namna fulani katika ulimwengu wenye giza, bali si katika giza. Tunafuata tu Nuru inapoenda, ndipo tunaifuata hiyo Nuru.

4 Na Baba yetu wa Mbinguni labda alikuwa na kitu ambacho hatujui kitu juu yake. Huenda kulikuwa na hatari kule juu. Ama, tena, huenda Yeye anamshughulikia mtu amlete. Mnaona, Mungu anaweza tu kutenda kazi na mtu mmoja namna hiyo; Yeye anaweza kubadilisha taifa zima kwa ajili ya mtu huyo mmoja tu, kuwaingiza. Na kwa hiyo tunajua yote yailikuwa kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Nasi tunamshukuru kwa jambo hilo, na kwa kutulinda. Na kulikuwa na wengi sisi . . .

5 Mimi pamoja na Billy tulisaidia kuwachukua, kote barabarani na mambo kama hayo, ya watu waliokuwa wamevunjwa-vunjwa na kila kitu. Bali tulifaulu bila shida. Tulitoka barabarani mara moja, bali hiyo ilikuwa tu kwa muda kidogo. Na mtu fulani kule juu, kwenye ranchi alishuka akaja akatuvuta kwa tingatinga. Kuteleza tu; kulikuwa kumeteleza sana.

6 Na yalikuwa moja ya mambo ambayo hawajakuwa nayo kwa . . . Wasingeweza, watu wa zamani wasingeweza kukumbuka kupata kuwa na tufani kama hiyo, katika nchi hiyo, wakati huo wa mwaka, Roundup, Montana. Nasi tulikuwa . . . Tunajua ya kwamba cho chote ambacho ni dhahiri hivyo, Bwana wetu alikuwa ameweka mkono Wake mle mahali fulani. Ilikuwa kwa ajili ya kusudi fulani, kwa—kwa ajili ya manufaa yetu. Kwa ajili ya manufaa yetu, hivyo ndivyo ilivyokuwa.

7 Na kwa hiyo nilimpigia simu Ndugu Neville, baada ya kurudi, nikasema, "Nitakuwa nyumbani Jumapili. Basi—basi kama ungetaka nishuke nije na labda niwe na shule ya Jumapili, naam, vema." Ndipo nikasema, "Basi nita . . . nami nitafurahi sana kuja."

8 Akasema, "Mbona, bila shaka, Ndugu Bill." Kasema, "Daima tunafurahia sana kuja kwako," kwa moyo mkunjufu mno na kukaribishwa, namna hiyo. Na kuweka jambo hilo kwenye kipindi chake cha redio, jana. Kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya mambo haya yote.

9 Basi asubuhi hii, sasa, kwa kuwa ni Sikukuu ya Mama. Karibu watu wote, mtasikia mahubiri ya Sikukuu ya Mama kila mahali, na watu wakizungumza juu ya mama, jambo ambalo nafikiri ni zuri sana. Tuachie jambo hilo ibada iliyosalia.

10 Asubuhi hii, nilikuwa nimetangaza, ya kwamba, so—somo la: *Kuvamiwa Kwa Marekani*, ambalo nilitaka kulizungumzia. Ambapo, labda mmesikia matangazo yenu ya redio, na mtasikia mengi ya hayo leo. Na kutakuwa na mahubiri ya Sikukuu ya Mama, labda, usiku wa leo kwenye ibada. Na kwa hiyo nilifikiri, asubuhi ya leo, ningetangaza, "ku-kuvamiwa."

11 Nilizungumza juu yake huko Denver, hapa, si kwa namna hasa ninayonuia kuutoa asubuhi hii, Mungu akipenda. Na, hilo, nilikuwa na wakati mzuri sana nalo. Bwana kweli alibariki kwa njia ya ajabu sana. Kwa namna fulani hilo mara kwa mara linatupa . . .

12 Inawabidi kutikiswa kidogo tu, kutambua maana ya jambo hilo lote, sivyo, wakati mwingine? Nasi tunaomba ya kwamba Mungu atatenda jambo hilo.

13 Basi, jambo lingine, kule, tulipomaliza . . . Wafanyi Biashara wa Denver ndio walioudhamini huo mkutano, na kulikuwa kudhamini tofauti kidogo na nilikowahi kudhaminiwa hapo awali.

14 Na kwa kawaida, wahudumu, wanapoidhamini mikutano, watasema . . . Mliutangaza? "Naam, kwa kanisa." Ni jambo kama hilo tu. Hao ni wachungaji; wanataka kundi lao kujua habari zake. Hiyo ni nini hii tu . . . Hiyo ni kazi yao.

15 Bali Wafanya Biashara walikuwa tofauti kidogo. Walitaka ulimwengu kujua jambo hilo, kwa hiyo wakatoa kwa moyo

mkunjufu yapata dola elfu tatu ama elfu nne za kutangazia kwenye motokaa zote za mitaani, teksi, milingoti yote ya motokaa, na kila mahali. Tulikuwa na wakati mzuri sana.

16 Baada ya ibada kwisha, waliniita kando, kasema, “Ndugu Branham, tukufanyie nini sasa? Unatuwia nini?”

17 Nikasema, “Mbona, bila shaka, hakuna cho chote.” Nikasema, “Siwawii cho chote.” Nikasema, “Mnaweza kulipia bili yangu ya hoteli, hapa chini, mkitaka.”

18 “Loo, tunataka kukufanyia kitu fulani.” Nao wasinge-. . . Nisingechukua cho chote kutoka kwao.

19 Kwa hiyo msimamizi akawaita. Akasema, “Ninaamini kwa namna fulani anapenda kuwinda na kuvua samaki, sivyo?”

Kasema, “Naam.”

20 Kwa hiyo mmoja wa hao wafanyi biashara alikuwa na ranchi kule, ndipo akasema, “Nitampa tu zawadi hiyo.”

21 Vema, Bw. Moore akapanda akaenda kuiona, naye ilimbidi kurudi yapata maili thelathini na tano, kwa farasi. Nikasema . . . Bw. Moore akasema, “Ningetaka kumwona Dada Branham amepanda farasi, akirudi huko.” Kwa hiyo yeye, wao, na . . .

22 Lakini, baada ya jambo hilo, hata hivyo, wakapanda wakaenda kwenye nyumba fulani kule Silver Plume, Colorado. Hii inapaswa kuwa upande huu sasa. Nao wakanunua ranchi ndogo kule, nao wanajenga nyumba yenye vyumba vitano kule kwa ajili yangu sasa, pia, kwenye Silver Plume, Colorado, ambayo iko katikati ya milima kabisa. Kwa hiyo, ninyi wavuvi, nadhani ni wakati unaofaa, kwa hiyo patakuwa ni mahali pazuri pa kupumzika, na wakati baada ya mikutano na kadhalika, Mungu akiruhusu. Hiyo ni juu Yake, mnaona.

23 Nataka sasa tuelekee kwenye Neno. Nami napenda tu Neno, Neno hai la Mungu. Ni, ndani ya Neno kuna Uzima. Naam, “Neno, andiko, huua, bali Roho hutoa Uzima.” Nao Uzima umo katika Neno, kwa maana ni Neno la Mungu. Uzima umo katika Neno Lake.

Kama niliwaambia, “Ninawapa . . . ”

24 Unasema, “Mimi nina njaa, asubuhi ya leo, Ndugu Branham. Waweza kunipa dola tano?”

25 Ningesema, “Nitakupa.” Basi kuna uhai wa kutosha katika jambo hilo kama kulivyo katika ahadi yangu.

26 Hivyo ndivyo ilivyo kwa Mungu. Mungu anapoahidi jambo lo lote, basi kile Mungu alicho, nini hii Yake . . . Hana budi kuwa katika Neno Lake. Mnaona? Neno hili halina . . . Neno hili ni sawa tu na Mungu. Ni Mungu.

27 Wewe ni kama Neno lako. Ni dhamana yako; ndivyo tulivyozoea kuliita. Dhamana yako ni neno lako. Kama hatuwezi kuliamini neno lako, basi siwezi kutumaini. Bali kama ninaweza

kuamini neno lako kwa ajili ya jambo lo lote, basi ni mtu muungwana.

28 Nayo Biblia ilisema, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu." Mnaona? Mnaona? "Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu."

29 Kama tungeweza kuwaza, ni dunia ile ile tunamoishi, asubuhi ya leo, ni Neno la Mungu. Mti *ule* ni Neno la Mungu. Nawe, mwili wako, ni Neno la Mungu. Mungu aliunena ukawa namna hiyo, akaufanya kutokana na kitu kisichokuwepo; ambacho hakikuwa na kitu.

30 Hivi mliwahi kuona maisha ya mwanadamu, mahali yanapotoka? Chembechembe moja ndogo, ndogo sana hata jicho la mwanadamu lisingeweza kuiona; ila tu kwa darubini kubwa, yenye nguvu. Na kutoka huko anatokea mtu mwenye uzito wa ratili mia moja hamsini, mia mbili. Ilitoka wapi? Mnaona? Mungu aliinena tu, nayo ikaanza tu, kwa asili, kukua, na hapo ikazaa kitu chenyewe. Yeye alinena kila mti, kila kitu, kikawa. Basi ni jambo la ajabu, ajabu sana, asubuhi ya leo, kuangalia Neno la Mungu.

31 Sasa jambo hili, asubuhi ya leo, katika Agano la Kale, tukifungua kwenye Mambo ya Nyakati. Nimekuwa tu nina wasiwasi kidogo . . . Wakati mnafungua sasa Mambo ya Nyakati, sura ya 18. Nimechoka kidogo. Lakini Bwana akipenda . . .

32 Sina hakika; tutajua zaidi Jumatano usiku. Bwana akipenda, na kanisa likijisikia likiongozwa namna hiyo, ningetaka kuchukua Jumatano, Alhamisi, Ijumaa, Jumamosi, na Jumapili, kama ufufuo hapa, ufufuo tu wa kufundisha kutoka kwenye Neno. [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Jumatano, Alhamisi, Ijumaa, Jumamosi, na Jumapili, kufundisha tu juu ya Neno; si ibada za kuponya, bali mafundisho. Labda Bwana atatuongoza namna hiyo. Halafu sisi . . . Ninapenda tu kuwa pamoja nanyi na kuwa na ushirika kwenye Neno, pamoja nanyi. Asanteni, sana, kwa ajili ya "amina" hiyo nzuri, nzuri sana.

33 Sasa katika sura ya 18 ya Mambo ya Nyakati, na kuanzia aya ya 12, tungetaka kuweka mawazo yetu kwenye msingi, kwa muda kidogo tu juu ya somo hili muhimu sana la zamani hizi. Mambo ya Nyaka- . . . Ama, Mambo ya Nyakati ya Pili, samahani. Mambo ya Nyakati ya Pili 18:12, nasi tutasoma sehemu yake hapa, tuone kile Bwana wetu atatutaka tujue.

> *Na yule mjumbe, aliyekwenda kumwita Mikaya, akamwambia, akasema, Angalia, maneno ya manabii kwa kinywa kimoja yasema mema kwa mfalme; neno lako basi na liwe kama mojawapo lao, ukaseme mema.*
>
> *Mikaya akasema, Kama aishivyo BWANA, neno lile atakalolinena Mungu wangu, ndilo nitakalolinena.*

Na alipokuja kwa mfalme, mfalme akamwambia, Je! Mikaya, tuende Ramothi-gileadi vitani, au tuache? Akasema, Kweeni, mkafanikiwe; nao watatiwa mikononi mwenu.

34 Sasa kuweka msingi wazo letu kwa muda kidogo; neno moja tu Kwake tena, juu ya jambo hili.

35 Baba yetu wa Mbinguni, kwa mioyo yenye shukrani tunakukaribia Wewe hivi sasa, kwa niaba ya nafsi zilizopotea, kwa niaba ya wale walio wahitaji, kwa niaba ya kanisa. Kwenye . . . Jalia Roho Mtakatifu aingie kwenye Neno upesi sasa, tunaomba. Lichukue uliingize moja kwa moja kwenye kila moyo hapa ulio na haja. Na wakati Yeye anapotoa Ujumbe Wake wa nguvu za Neno moyoni, sisi sote na tufanikiwe Kwake, asubuhi hii; tukienda, tukiondoka maskanini, tukifurahi na kumsifu Mungu, tukisema, "Mioyo yetu inawaka ndani yetu kwa ajili ya Uwepo Wake." Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

36 Mandhari yetu yana msingi wake, asubuhi ya leo, juu ya jambo la msiba. Nalo Agano la Kale, kwangu mimi, daima ni kivuli ama u—utabiri wa mbele wa Agano Jipya. Mara nyingi, mtu fulani amesema, "Ndugu Branham, kwa nini daima unachukua Agano la Kale? Karibu kila wakati, ukichukua fungu la maneno, utarudi kwenye Angano la Kale." Ninafanya hivyo kwa sababu ninapenda kufananisha. Ninapenda . . .

37 Elimu yangu ni haba sana, kama wote wajuavyo. Na jinsi tu ninavyojua kwamba niko karibu na kuwa sahihi, ni kuona jinsi mfano ulivyokuwa, kuangalia kwenye ramani na kuona jinsi ilivyokuwa. Ndipo ninajua kile *hicho* kilivyokuwa kitakuwa kitu fulani kinachofanana na *hiki* hapa, kwa maana ni kivuli chake tu. Nami daima huangalia nyuma kwenye Agano la Kale kuona kile wana wa Israeli walichofanya, kuona adhabu ya dhambi ilikuwa nini, kuona haki ya manabii ilikuwa nini, kuona mambo hayo yote yalivyokuwa; ndipo nitakuwa na fununu *hiki* ni kitu gani hapa, ambacho kimetangulia kuonyesha katika kivuli kile kitakachokuwa katika jumla ya matokeo mwishoni.

38 Katika wakati huu, kulikwisha kuwa na jambo kubwa lililotukia kwa Israeli. Ilikuwa katika giza la usiku wao wa manane.

39 Katika Agano la Kale, Bwana akipenda, labda katika ibada zijazo, ningetaka kuoyesha jinsi zile Nyakati Saba za Kanisa zilivyoonyeshwa kwa mfano katika Agano la Kale. Jinsi zilivyoanza hasa kama hapo—hapo mwanzo wa Nyakati za Kanisa za kanisa la Mataifa, kisha zikashuka moja kwa moja kupitia wakati wa giza kama huo, kisha zikatokeza zikaingia kwenye wakati wa fahari wa Pentekoste, kwenye kule kushuka kwa Roho Mtakatifu katika kanisa la mwanzoni la . . . katika majira ya Kiyahudi. Kisha zikapitia kwenye kipindi kingine cha kanisa la Mataifa, kupitia kwenye wakati wa giza, kisha

zikatokeza tena zikaingia katika ile Milki ya Miaka Elfu Moja, mwishoni.

40 Naam, jinsi ambavyo huko nyuma kwenye zile karne za katikati kule, huyu mfalme mkuu Ahabu alivyoingia kwenye mamlaka. Naye kwa namna fulani alikuwa anatumia sifa za wafalme wengine wa Israeli, ambao walikuwa. . . Ahabu, mwenyewe, alikuwa kwa namna fulani mwa—mwamini wa mpakani. Mimi daima nimemtaja namna hiyo, kwa maana yeye wakati mmoja alikuwa wa upande *huu* wa ua, wakati mwingine upande *ule* wa ua.

41 Usingejua mahali pa kusimama, mtu kigeugeu kama huyo. Ama, mtu anayekiri kuwa Mkristo, na huku ni kigeugeu namna hiyo, hujui la kufanya juu ya huyo mtu. Leo wao ni Wakristo; kesho hujui waliko. Kanisani leo, wanafurahi na kuimba na kumsifu Mungu; na kesho, wako huko nje wakinywa pombe, wakilewa, na kuzurura kila mahali. Basi mtu wa namna hiyo ni vigumu kufanya lo lote naye.

42 Ninakumbuka, nilipokuwa kijana mdogo, wakati mmoja tulikuwa na fa—farasi mzee, aliyekuwa anaruka ua kila wakati. Nami nakisia wengi wenu wanaume, rika langu, mngejua huko nyuma katika siku hizo za farasi, siku za magari ya farasi. Nimekuja mara nyingi, moja kwa moja kushuka kwenye mtaa huu hapa, nimempanda farasi na gari lake, mimi mwenyewe. Nina umri wa miaka arobaini na mitano. Kwa hiyo, wao, wanakumbuka. . . Farasi huyu mzee, tungeweka nira shingoni mwake, kama vile ungemwekea ng'ombe, na kumzuia asiruke ua. Naye angeruka, hata hivyo. Naye angening'iniza hiyo nira na kugeuka, na kadhalika. Angeruka juu ya huo ua. Basi siku moja, kile ali-. . .

43 Nilishangaa ni kitu gani kilichokuwa kinamvutia maskini jamaa huyo. Basi kulikuwa na shimo kubwa kule chini. Sasa alikuwa amesimama katika majani ya alfalfa, kubwa, bali alikuwa anataka. . . Kulikuwa na majani ya nyasi za shamba la matunda kwenye shimo la takataka. Basi aliruka ua ule akaingia kwenye lile shimo la taka ambamo waya hizi zote na glasi. Vema, alikuwa kwenye jaa le-letu la taka, kisha akaingia mle ndani kupata mego chache za nyasi hizo za shamba la matunda. Nasi ilitubidi kuwachukua farasi wachache na kumvuta kutoka kwenye shimo hilo la taka. Alipoingia mle ndani, alining'inia. Na wakati aliposimama kule nje, alikuwa anatetemeka na kutokwa na damu, na—na jinsi alivyokuwa, kupata tu mego moja, ama mbili, za hizo nyasi za shamba la matunda, na huku alikuwa amesimama kwenye majani ya alfalfa, yaliyokuwa karibu kufikia magotini mwake.

44 Mara nyingi nimefikiria juu ya picha hiyo. "Njia ya mtu asiye haki ni ngumu." Yeye asingetulia tu mahali alipokuwa anakula na kuwa na wakati mzuri sana, lakini ile. . . ilimbidi kuruka

ua aende akachubuliwe-chebuliwe na kukatwa-katwa namna hiyo, kusudi apate tu mego la—la nyasi ya namna nyingine. Sasa hivyo karibu ni kama tu watu wanavyofanya, wanaoruka ua la malisho ya Mungu. Hivi hamwamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Wanatoka, wanatoka leo; wanaingia. Wako kanisani, wakiwa na wakati mzuri sana; kisha, kesho, wanajiuza kwa kitu kama hicho. Linalifanya jambo hilo kuwa gumu sana.

45 Ama Ahabu alikuwa kwa namna fulani mtu wa namna hiyo. Kila upande upepo ulikovuma, Ahabu alitweka tanga lake, kama ulikuwa upande *huu* ama upande *ule*. Ndoa yake ilimchafua kabisa, akiwa na maskini mwanamke aliyekuwa binti mdogo wa mfalme, binti mfalme, Yezebeli fulani. Mrembo sana ukimwangalia, mwanamke mrembo sana, lakini moyoni mwake alikuwa mwovu sana. Naye alikuwa mwabudu sanamu, na aliwafanya Israeli wote . . .

46 Naam, jinsi ningetaka kufikia hapo kwa dakika chache tu, tulikuwa, na kufikia kwenye kiini cha jambo hili juu ya umama, mnaona, pale. Basi wakati mwanamume anapoanza kuoa; namna ya msichana, mwanamke ambaye yeye . . . Ni zaidi ya kuangalia tu urembo. Huna budi kupata mtu fulani, nafsi na mwili vimeunganishwa pamoja; mtu atakayekuwa rafiki na mwenzio kweli, atakayekaa pamoja nawe katika heri na shari.

47 Naam, bali, Ahabu, yeye alivutiwa naye tu kwa sababu alikuwa mrembo, nafikiri, ndipo akamwoa. Isingekuwa kitu kingine kwake, kwa kuwa alikuwa mwovu sana. Basi akaja kule. Halafu, bila shaka, kwa kuwa alikuwa ameshikamana naye namna hiyo, na alimpenda, mbona, alisababisha Israeli yote kutenda dhambi na kuwa kinyume cha Mungu, na kuharibu madhabahu za Mungu; akajenga madhabahu za Baali. Nao walikuwa na ibada za Baali kila mahali katika Israeli, wakati huo.

48 Basi, alikuwa na, mkewe, naye alikuwa amemfanya Nabothi mwenye haki . . . Wengi wenu mmesoma habari zake. Jinsi alivyolichukua shamba lake, kwa udanganyifu; kisha akaapa, uongo, na alikuwa na mashahidi wa uongo dhidi yake. Kwa maana, yeye alitaka kufanya jambo fulani kwa ajili ya mumewe; basi akamwua mtu mwenye haki, ili apate shamba lililopakana na shamba la ikulu.

49 Yote haya, Mungu alikuwa anaangalia. Kwa hiyo nabii, Eliya, aliyekuwa mtumishi mkuu, mwenye nguvu wa Bwana, alitabiri na kumwambia Yezebeli yatakayompata. Naye akamwambia Ahabu kwamba mbwa wangeiramba damu yake mwenyewe. Naam, Mungu akiwa amesema jambo lo lote . . . Bila shaka, siku hizo, Neno la Moja kwa moja la Bwana lilikuja kupitia kwa nabii.

50 “Mungu, kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi alisema na baba zetu katika manabii, katika siku hizi za mwisho katika Mwanawe, Yesu Kristo.”

51 Kwa hiyo, *Hili* ndilo Neno. Na iwapo kitu cho chote ni kinyume cha Hilo, kiache. Mnaona? Naam, kwa njia nyingine, Yeye anasema siku hizi katika nabii, mwonaji, na kadhalika. Lakini kwanza ni *Hili*, Neno, sasa.

52 Basi Ahabu alikuwa amefanya uovu huu. Kisha akaendelea; Mungu akiwabariki watu kwa miaka mingi. Ndipo, hatimaye, Yehoshafati alikuwa mfalme wa Yuda, huku Ahabu akiwa mfalme wa Israeli.

53 Ndipo, basi, Yohashafati alikuwa mtu mwenye haki. Alikuwa mwana wa Asa. Asa alikuwa mtu mwe—mwenye haki, naye akaharibu madhabahu zote za—za sanamu; akajenga madhabahu za Yehova. Nao walikuwa na u—ufufuo, kama ilivyokuwa, huko katika Yuda. Kisha baada ya kitambo kidogo, Yehoshafati ama . . .

54 Ahabu, hasa, akatuma, naye akapata kipande kingine cha ardhi, katika Ashuri, alichodhani kilikuwa chake, alichodhani angeenda akakichukue. Kwa hiyo akamwuliza huyu Yehoshafati iwapo angekuja na kufanya mapatano naye.

55 Ndipo, bila shaka, kuna hatari kubwa sasa, mnaona, walipomwona mfalme huyu mkuu, Ahabu, kule chini, nao wakamwona huyu mkubwa huku juu, Yehoshafati; mmoja wao, mwenye uvuguvugu; yule mwingine, mtu aliyejazwa na Roho. Angalia jinsi unavyofanya mapatano yako. Angalia unalotenda, jinsi unavyojifunga nira pamoja na wasioamini. Jiweke ukiwa msafi, hasa sana katika siku tunayoishi.

56 Ninaamini, kanisa, bila shaka yo yote, jambo hili limechoma moyo wangu. Hiyo ndiyo sababu ninatazamia siku hizi tano usiku, hivi karibuni; ili mara moja tena, kabla halijatukia, kulichambua kanisa hili kwelikweli, kwa Biblia.

57 Tunaishi katika vivuli vya wakati. Ingeweza kutukia wakati wo wote. Tunapoona wakati umewadia kwa mambo kutukia; uovu hasa wa adui, zile nguvu hasa. Tunaangalia mvua hizi kubwa za theluji na kila kitu kikitukia, tauni hizi zote, mambo yote mbalimbali. Hizo zote zinasababishwa na vurugu hizi, kurusha mbomu hizi na kadhalika. Wao wanavuruga mambo yote hapa. Nao wanavuruga mambo katika chumba kikubwa cha Mungu cha utafiti, kulitimiza Neno Lake. Itatendeka.

58 Kwa hiyo, “mtu wa kuasi” anainuka, utawala, mdanganyifu sana. Jamani! Nilimsikia mhudumu asubuhi ya leo, mtu aliyejazwa na Roho, akichukua alama ya mnyama na kusema kwamba mpinga Kristo alikuwa ni Urusi. Ni kosa jinsi gani! A-ha! Urusi haina uhusiano wo wote na jambo hilo. La, bwana. Hiyo ni Kimaandiko. Naam, lakini angalia katika wakati huu mkuu tunaoishi, onyo.

59 Naam, Yohoshafati huyu, akijisikia vizuri kwa namna fulani kwa maana yule mfalme mwenye nguvu wa Israeli alisema, "Njoo, ukanitembelee." Basi akashuka akaenda kule. Nao wakachukua maksai na kondoo, na kadhalika, wakatoa dhabihu. Wakati wote, katika moyo wa Ahabu kule chini, alikuwa mdanganyifu, maana hakuwa anamwabudu Huyo, wala kutoa sadaka hao kondoo na kadhalika kwa moyo mwaminifu, kwa maana, hata hivyo, yeye aliegemea zaidi kwenye dini ya mkewe.

60 Basi angalia, kama vile tu Ahabu alivyomwoa Yezebeli katika wakati wa ule wakati mkuu wa giza wa Israeli, aliingiza ibada ya sanamu katika Israeli, mfano halisi wa siku hizi. Katika wakati tu wa giza; wakati tulipotoka kupitia katika wale mitume wa mwanzoni, zamu ya pili, zamu ya tatu, tukaingia kwenye wakati wa giza, miaka elfu moja na mia tano. Kama tu vile Ahabu alivyomwoa Yezebeli na kuleta ibada za sanamu katika Israeli, vivyo hivyo kanisa la Roho Mtakatifu lilioana na itikadi, na kurudisha ibada za sanamu, na leo ni mfano wa Ukristo. Mnaona? Mnaona, ni giza sana! Na sasa inazidi kuendelea, kila siku; kila wakati wa kanisa unashuka kwenye jambo lile lile, kufikia kile kipeo kikuu, na hali ya uvuguvugu inaingia, Wakati wa Kanisa la Laodikia wenye uvuguvugu! Loo, ni wakati wa kuchukiza jinsi gani tunaoishi!

61 Sikilizeni. Ninataka kukiri papa hapa, kabla sijaenda umbali wo wote ule. Mimi ni mhubiri wa mtindo wa zamani ambaye anatamani kuziona zile siku za kale tena. Nimeona mengi sana ya huu uigaji, Hollywood ikiirembesha Injili, hata nimechukizwa na kuchoshwa nayo. Naam, bwana. Ninataka kuona ile ya mtindo wa kale. Ninasikitika tunaufanya Ukristo kuwa mrembo mno kwa watu; mstari wa hatari.

62 Sasa Yehoshafati anashuka anakuja, anawaza, "Loo, vema, mfalme huyu mkuu wa Israeli, mimi nitanini hii tu . . . Loo, sisi tuta- . . . Itakuwa sawa." Na moja kwa moja katikakati ya kiinimacho hiki kikubwa, alifanya nini? Alifanya mapatano, kukwea kwenda kupigana na adui, katika msimamo wa pamoja, kwa maana wao walisema, "Sote wawili ni watu wale wale." Lakini wao hawakuwa namna hiyo. Moja lilikuwa kundi lililojazwa na Roho, hilo lingine lilikuwa kundi lenye uvuguvugu. Wao si watu wa namna ile ile. La, bwana. Huwezi kuwa . . .

63 Giza haliwezi kushirikiana na nuru. U—usiku hauwezi kukaa katika uwepo wa nuru ya jua. Na wakati mdanganyifu sana uliopo ni katikati ya nyakati hizo. Wakati tu jua linaposhuka ama kuchomoza, ndio wakati mdanganyifu sana uliopo. Hakuna uwezo wa kuona vizuri; taa zako katika motokaa yako hazitaonyesha vizuri na dhahiri. Afadhali kuwe na giza ama nuru. Yesu alisema, "Iweni moto ama baridi, si wenye uvuguvugu." Basi, huo ndio mstari wa hatari.

64 Kisha Yehoshafati, aliposhuka akaja, ndipo mwungano huu mkubwa ukafanywa, ambao haukumpendeza Mungu. Tena angalia, katika wakati wake tu, kusisimka kwote sasa, "Nimepata kibali kwa mfalme huyu. Basi, loo, ni—ni—nina ushirika na jirani huyu. Nina . . . "

65 Mnaona, iweni waangalifu, kwa jambo hilo, enyi kanisa! Mnaona? Hilo ndilo linalosababisha shida yote kwenye maskani hii hapa, na katika nyingine. Mnaona? Iweni waangalifu juu ya kile mnachochanganyikana nacho. Mnaona? Tokeni moja kwa moja nje, kisha mwe upande wa Kristo ama mwe kinyume Chake. Mnaona?

66 Naam, jamaa huyu alifanya mapatano, naye alifikiri alikuwa amefanya jambo kubwa. Hata hivyo, wakati aliposema, "Hivi hakuna sasa, kabla hatujakwea, hivi haitubidi kumtaka shauri Bwana juu ya jambo hili?" Naam, Yehoshafati alikuwa amesaza dini ya kutosha ndani ya nafsi yake, katika kosa lake, kwamba alikuwa ameshuka akaenda kule kwa mfalme huyu, lakini alikuwa amesaza dini ya kutosha kuwaza, "Vema, tunapaswa angaa kumtaka shauri Bwana."

67 Naam, Ahabu alikuwa anaenda moja kwa moja bila kusema neno; njia yake tu ya kutofikiria, ya kimwili na ya kibinadamu ya kufanya mambo.

68 Nashangaa tu papa hapa, enyi kanisa, kama jambo hilo halijatukia, mara nyingi, tumefanya makosa. Kuliwazia, na kusema, "Vema, inapaswa kuwa namna *hii*," na tunalifanya namna hiyo.

69 Nafikiri hapo ndipo kundi nzima la Uijilisti wa Kimarekani lilipo leo, kwamba tumeliweka katika mfano wa—wa, ningesema, uinjilisti wa Hollywood, zaidi sana juu ya viinimacho. Tunaona mwinjilisti anakuja jukwaani, leo, na, jamani, anajigamba kabisa, na kufanya mizaha chungu nzima kabla hajaanza kuhubiri, na mambo kama hayo, na kufanya yasiyofaa na kutenda kama mcheshi, mimbarani. Inapofikia wakati wa kutoa wito wa madhabahuni, watu hata hawaoni unyenyekevu wo wote wa kutolea wito wa madhabahuni. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo sababu ulimwengu umeingia katika hali ya uvuguvugu leo, uliomo ndani yake.

70 Sijui, leo. Ni kwamba tu, leo, mimi . . . Kanisa, tumejaribu kuwapeleka wavulana wetu shuleni, kusoma saikolojia, na kadhalika namna hiyo, kujua jinsi ya kutayarisha orodha ya mambo, kwenda mimbarani na kutayarisha nini hii yetu . . . Ujumbe unashawishi sana, hata utawashika watu, na kuvutia usikivu wao. Na wanasaikolojia wengi wanatoka wanaenda kama waalimu namna hiyo, na kuigiza kutia mambo fulani kadha wa kadha. Nami nashangaa tu, wakati wao . . . Daima tunawaambia uzuri na mvuto wa kanisa. Bali tunashindwa kuwaambia, "Yeye atakayenifuata Mimi, na

ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake anifuate Mimi." Sijui kama hatujaufanya uzuri wa kanisa kuwa wenye kuvutia kupita kiasi, kwa jamaa anayeingia.

71 Kwa mfano, kanisa la Kibatisti leo lina msemo, "Milioni moja zaidi katika mwaka wa "44," wakiwaingiza wafuasi kwa maelfu, na makumi elfu, wasioongolewa, watu tu wanaoingia na kujiunga na kanisa. Na jambo hilo ni la aibu kwa Kanisa la Yesu Kristo, kuwaingiza wafuasi kama hao. Wangali wanakuywa pombe. Wangali wanavuta sigara. Wangali wanacheza karata. Wangali wanasema uongo.

72 Wao wanakuja kanisani, wakitazamia kutumbuizwa na kundi la wainjilisti wa Hollywood wanaoinuka, wanatia viinamacho chungu nzima, na zana nyingi kubwa zimewekwa huku na huko jukwaani.

73 Wakati, wao wanapaswa kuwa na wito wa madhabahuni wa mtindo wa zamani, wa Mungu kwanza, wa kulia sana hapo chini; ambapo wanawake na wanaume hawaji kufanya viinimacho, ama kukimbia kule na kutenda kama mcheshi, bali kushuka kwenda madhabahuni na kutambua ya kwamba mauti ya Yesu Kristo pale, aliyewafia, ya kwamba wao wanarudi wakiwa waaminifu kwa Mungu tena.

74 Sijui kama hatuishi katika wakati wa namna hiyo, wakati tunapowachukua wainjilisti wakuu, kama wengi wanaovuka nchi leo, waijilisti wakuu wenye sifa ambao wamesoma saikolojia na wanawavutia watu kanisani. Lakini ukisha waingiza kanisani, basi utawafanyia kitu gani? Ita—itakuwaje baada ya wao kuingia kanisani? Wanajiunga tu na kanisa, na kurudi na dhambi ile ile na tamaa ile ile waliyokuja kanisani nayo. Wanarudi vile vile walivyokuja. Na hiyo ndiyo sababu, leo, ulimwengu unazidi kuangalia, kasema, "Vema, kama mtu huyo ana dini, kama mtu *huyu* ana dini . . . "

75 Nasikitika tumefanya jambo hilo rahisi sana. Ni, napenda . . . Nafikiri, furaha, bila shaka, ninaamini ya kwamba furaha zote zimo katika Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Ninaamini ni shangwe na furaha. Lakini kumbuka, ewe ndugu, ni njia ya maumivu makuu na mateso na msalaba. Huna budi kutambua jambo hilo, pia. Hiyo ni kweli. Sijui kama hatukuchora kidogo zaidi—kidogo laini zaidi kupita kiasi.

76 Nilikuwa nikitazama, na mke wangu akaweka . . . Akaanza kutoka, ndipo akaweka waridi kwenye koti langu asubuhi ya leo. Akasema, "Unapaswa kulivaa. Mamako yu hai."

Nami nikasema, "Loo, mpenzi, sijui."

77 Sikukuu ya Mama ni nzuri sana, lakini jambo hilo ni kama ulimwengu, wamelifanya jambo la biashara, kuuza tu maua na mambo kama hayo. Mbona, ni kumwaibisha mama. Mbona, mama yangu ni mama yangu kila siku ya mwaka, naam, bwana, si siku moja tu.

Nitasema, “Hivi unampenda mama yako?”

78 “Nilimtumia shada la maua kwenye Sikukuu iliyopita ya Mama.” Vema, ndugu, yeye anapaswa kuwa mama kila siku. Lakini jambo hilo ni la kibiashara.

79 Ua hilo ni zuri. Mimi napenda ua zuri. Ninafikiria juu ya jambo hilo kama ninavyofanya... Jinsi hilo ua lilivyo zuri! Linastawi. Pia lina harufu nzuri. Na mpitaji hulinusia. Mnyama anapita pale, analinusia. Lakini, sasa angalia, linapendeza. Kama vile Kanisa la Bwana Yesu Kristo, ni Jambo tukufu sana; kuponya Kiungu, na nguvu, na maajabu, na ishara, na miujiza, na uhuru kutokana na dhambi. Ni mahali papendezapo. Lakini, angalia, kama waridi hilo... Itatubidi kuja, Kanisa, kama vile maumbile yote.

80 Waridi hilo, kwa kuwa ni zuri, kila ng’ombe nchini angeliramba kama angeweza. Lakini maumbile yametoa singe ndogo, mikuki midogo inayotokeza pale, inayoitwa miiba, nao wanaliacha. Hiyo inalilinda. Hiyo ni kweli kabisa.

81 Nami nafikiri, leo, kama hatuna Neno la Mungu, lililo kali kuliko upanga ukatao kuwili, kuuzunguka uzuri wa nguvu za utakatifu wa Mungu, tutamwacha kila ng’ombe nchini alirambe na kulichuma. Atalitia mate ovyo ovyo. Itakuwa ni aibu kwa Kanisa. Hiyo ni kweli.

82 Nafikiri, leo, tunachohitaji ni wahudumu zaidi wa mtindo wa kale, walioitwa na Mungu, wabichi, labda si wenye elimu nyingi, bali watawaleta watu kwenye madhabahu, na kule wapate kuugua. Si kwa furaha na kucheka, wakifanya vishindo kwa switi ngamu, na kuandika jina lao kwenye kijikaratasi; lakini, ewe ndugu, kulia kwa kale na kufa, mpaka wanaume kwa wanawake wametubu kabisa dhambi zao na kumkaribia Mungu. Amina.

83 Ninawaambia, tuna, “Inueni mikono yenu, wanaotaka kumkubali Kristo,” yote namna hiyo. Hilo ni sawa, ndugu, lakini hilo hali—haliiondoi dhambi.

84 Huna budi kutubu kwanza, jiweke sawa, ushuke uende pale na ulie kweli. Ninaweza kukumbuka nyakati ambazo watu wa mtindo wa kale wangeshuka waje kwenye marefu ya kanisa, na huku na huko barabarani, wakilia, na kuzungumza na majirani wao. Hao walikuwa ni Wakristo wa siku hizo, wakiyasimulia mambo ya Bwana.

85 Basi, leo, tunaandika jina letu kwenye kitabu cha kanisa, kisha tunatoka na kukaa nyumbani, na tusiseme neno juu ya jambo Hilo. Hatujali! “Mradi tu sisi ni wafuasi wa kanisa, ni sawa.” Nina hakika sisi tumekosea pale, enyi watu. Chunguzeni! Kwa kuwa, hilo halitasimama kwenye Hukumu. La, bwana. Halitasimama.

86 Hakuna lingine, "Yeye atakayenifuata Mimi, na ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake, afe kila siku." Kaa ukiwa maiti, pale msalabani. Hiyo ni kweli. Kuugua! "Ile njia, nitafuata ile njia," mnaimba, "pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa."

87 Nafikiri leo, ni wakati wa namna gani tunaoishi! Huo, uinjilisti, wanautoa nje kwenye nuru kubwa mno zinazoangaza, nao wanajaribu... Unapomwona mwinjilisti akija mjini, unashangaa. Mimi, mikutano yangu imekuwa na hatia ya jambo lilo hilo. Hiyo ni kweli. Sijui ni nani anayekuja mjini, wakati mwingine, ni yule mwinjilisti ama ni Yesu Kristo? Mbona, wao wana-...

88 Nilienda mahali fulani hapa, si muda mrefu uliopita, ambapo mwinjilisti fulani alipaswa kuja. Nalo Jina la Yesu... Mbona, wao walikuwa na picha ya huyo mwijilisti, "mtu wa majira tunayoishi," mtu aliye na *hili*, mtu aliye na *lile*.

89 Mimi, wakati mwingine ninawazia juu ya huduma yangu, na kuwaona watu wakija. Nami ningeingia kwenye chumba cha hoteli, kasema, "Mungu, ni nani—ni nani watu wanakuja kuona, mimi ama Wewe?" Mnaona? "Kama wanakuja kuniona mimi, wamepotea, hata hivyo; lakini, Ee Mungu, nirarue, niondolee mbali. Ninataka kukuwakilisha Wewe, Yeye ambaye nitasimama mbele Yake siku moja, kwa mikono inayotetemeka na mwili unaotetemeka, mwili mnyonge, nikikutazama Wewe. Nikijua ya kwamba nafsi yangu inaning'inia kwa uamuzi wako." Na tumwinue Kristo.

90 Leo, mnasema, "Vema, mimi ni wa Kibatisti. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni wa maskani. Ninafanya jambo *hili*." Loo, hilo halina uhusiano na jambo hilo; si kitu. Nashangaa wakati mwigine.

91 Hapa si muda mrefu uliopita, niliona ta—tangazo limewekwa, ambapo kampeni fulani ilikuwa inakuja mjini. Na neno la huyo mtu, jina la huyo mtu liliandikwa kwa herufi kubwa mno kila mahali, namna *hiyo*. Na chini kabisa, kwenye kona ndogo, kasema, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele," kule chini kabisa pembeni. Mnaona?

92 Wao waliondoa utakatifu wote kutoka kwa Kristo, kisha wakauweka kwa mtu fulani, ama kanisa fulani, ama madhehebu fulani. Ndugu, ninakwambia, unaweza kufaulu kwa viinimacho na upumbavu wa Hollywood, namna hiyo, na ni kwa njia ya kanisa. Lakini, katika Uwepo wa Yesu Kristo, Yeye Ndiye anayepaswa kutukuzwa. Hiyo ni kweli. Sasa hiyo ni kweli, ndugu na dada yangu wapendwa.

93 Msinikasirikie. Kumbukeni tu ya kwamba ninawahubiria. Ninataka kuhubiri kama kwamba haya yalikuwa ndiyo mahubiri ya mwisho ningepata kuhubiri maishani mwangu. Ninataka kuhubiri, kila mahubiri ninayohubiri, kama kwamba

nilikuwa mtu anayekufa akiwahubiria watu wanaokufa. Na, mimi nafa; nuru yangu inafifia, kila siku; yako inafifia, pia. Nasi tu watu wanaopatikana na mauti. Nasi hatuna budi kumkabili Mungu aliye hai, moja ya siku hizi, nasi hatuna budi kuwa wanyenyekevu sana juu ya jambo hili.

94 Na kwa kiinimacho tu, na kufanya yasiyofaa, na kujiunga na kanisa, na kwenda *hapa* na *pale*, na kutenda *hivi* na *vile*.

95 Afadhali tuwe tukifanya mikutano ya maombi ya mtindo wa kale manyumbani mwetu, tukimlilia Mungu, mchana na usiku. Siku ile imekaribia, "wakati wa dhiki, wakati wa shida." Biblia ilisema, "siku yenye giza." Nasi tunaishi katika hiyo.

96 Jinsi mtu huyu mkuu alivyoshuka kwenda kule akiwa na mwamsho. Akajiunga na wenye uvuguvugu, pamoja na wa mpakani, na kufikiri alikuwa anafanya jambo kubwa, alidhani kwamba Mungu anambariki. Wala hakutambua kwamba papo hapo alikuwa anaingiza kundi hili lote pamoja naye. Ati nini? "Kundi letu dogo, la Yuda—la Yuda hapa, ligeshuka lije likajiunge na makundi makubwa ya Israeli. Jinsi tutakavyokuwa watu wenye nguvu!"

97 Naam basi. Na hiyo ndiyo jama Ibilisi anatumia hivi sasa, kumwingiza mpinga Kristo; dhahiri tu kama ninavyosimama kwenye kitu hiki. "Tutaunganisha jitihada zetu pamoja." Hatuwezi kufanya jambo hilo. Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana?

98 Marekani hii inafanya, kituko kile kile na kosa lile lile, wakati ilipojiunga na Urusi kule nyuma. Wakati huo walikuwa karibu kupigana vita, nasi tukajiunga pamoja na Urusi. Na sasa mnaona kile tulichopata, sivyo? Wao wana ndege zetu na siri zetu zote, na mabomu yetu ya atomiki na kila kitu kiko huko, kukilipua kiturudie sisi. Jambo lile lile linaambatana na mambo ya kiroho!

99 Halafu tunaona, baada ya Yehoshafati kufanya mwungano huu, nao wakafanya shauri. Sasa angalia, angalia ulimwengu wa nje, yeye alisema, "Hakika, tuna manabii wengi hapa chini. Tuna seminari iliyojaa wao."

100 Wao wanashuka wanakwenda kuwachukua jamaa ambao walikuwa wamefunzwa, waliojua saikolojia, waliojua mambo yote. Kasema, "Njoni sasa, nasi tunamwuliza na kumtaka shauri Bwana."

101 Wote hao, bila shaka, katika nia zao za kimwili zenye kiburi, wakapanda wakaja pale wakasema, "Naam, angalieni, sisi. . . Kweeni. Bwana yu pamoja nanyi, na Bwana atawapa sehemu hiyo ya ardhi kule. Hiyo, itakuwa yenu. Mtawasukuma Waashuri huko nyuma kabisa. Mtafanya jambo hilo." Mmoja wao hata alijitengenezea jozi moja kubwa ya pembe za chuma, kisha akaanza kukimbia kila mahali namna *hii*, akisema, "Hivi ndivyo! Mtawasukumia mbali Waashuri."

102 Lakini, Yehoshafati, alikuwa wa kiroho zaidi kidogo tu, kuvumilia upuzi huo wa kipumbavu! Hiyo ni kweli.

103 Mungu, tupe Yehoshafati wengine zaidi, tumechukizwa na kuchoshwa na upuzi huu wa Hollywood. Hiyo ni kweli, kujifanya, kujifanya wao ni kitu wasicho; wakijifanya, kuigiza, wakiwaingiza. Halafu wanapoingia, mlipata nini alipoingia? Kama vile kumwuliza mtu, "njoo uogelee," na ni jangwani. Hakuna kitu ila changarawe za ghuba kichwani mwako, kusababisha huzuni baadaye!

104 Sasa angalieni, unaweza kuwaingiza wapi? Bibi fulani aliniambia hivi majuzi, "Mwanamume fulani alisema, 'Ningeenda kanisani, lakini ninge—ningepata nini nikienda kanisani?' Kasema, 'Yote wanayofanya ni kutayarisha vyakula fulani vya jioni, na juu ya jambo *hili*, *lile*, na *linginelo*.'" Ndipo huyo bibi akasema, "Nilisimama nimeshangaa, kwa kuwa sikujua nimpeleke wapi." Naam basi. Kasema, "Laiti ningalipata kanisa la kale ambako wanaimba kweli kweli zile nyimbo za mtindo wa kale na kuishi kitauwa."

105 Watoto wakiwa na njaa, watakula kwenye pipa la takataka. Ni juu ya Kanisa la Mungu aliye hai kuwalisha Neno la kweli lililo hai la . . . la Mungu.

106 Pale, na viinimacho hivyo vyote na kadhalika; Yehoshafati alisema, "Hivi hakuna mmoja zaidi?"

107 "Mmoja zaidi?" kasema Ahabu. "Vema, unataka nini na mwingine zaidi? Tuna watu mia nne walio bora zaidi, waliochaguliwa, wenye elimu, waliolishwa vizuri, waliovalia nadhifu sana nchini, wamesimama hapa. Kila mmoja wao akiwa katika umoja, na moyo mmoja, na sauti moja, akisema, 'Nendeni, Mungu yu pamoja nanyi.'"

108 Sijui kama Marekani haijakutana na jambo lile lile! Sijui kama kanisa la Mungu halijakutana na jambo lile lile! Sijui. "Vema," kasema, "angalia, wao wanafanikiwa. Wanafanya mikutano mikubwa, mikubwa mno. Wanawachukua maelfu wakati mmoja." Bali sijui kama hakuna mmoja zaidi! Sijui kama hakuna kitu kingine tofauti!

109 Tunaona, tuna waongofu elfu thelathini katika majuma sita, na majuma sita baadaye hatuna mmoja. Kuna kasoro mahali fulani. Hiyo ni kweli. Na yote ni viinimacho, kujifanya. Ulimwengu, kupitia kwenye televisheni, kupitia kwenye redio, kupitia kwenye sinema, na milango hiyo pale, umeliharibu taifa hili kwa upuzi wa Hollywood. Hiyo ni kweli. Kila kitu kinataka kuwa katika kiinimacho kikubwa. Si hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnajua hiyo ni kweli. Hatua tena ile dini ya mtindo wa kale tuliyokuwa nayo miaka kadha iliyopita. Ni kwa sababu imeachwa. Tutafikia jambo hilo, katika muda kidogo tu, nanyi mtaona.

110 Naam, ni picha nzuri namna gani, ama picha ya kuvutia, ningesema. Basi huyu hapa Yehoshafati anakuja, kasema, "Naam, ninawaona wote. Wao, kila mmoja wao, wana digrii zao," na cho chote kilichokuwa. "Pia wao ni manabii. Wao ni wahudumu mashuhuri. Wametoka katika vyuo mashuhuri. Nao wote ni haya yote. Wao wametoka katika ile shule kubwa ya nabii, na kila kitu. Wote wana umoja. Hiyo ni kweli. Lakini hivi hakuna mmoja zaidi?"

111 "Vema, unahitaji mmoja zaidi wa nini, wakati mia nne wanatoa kibali chao kwa wakati mmoja?"

112 Lakini mtu huyo, kule chini kabisa katika moyo wake, alikuwa na Mungu. Naye alijua ya kwamba kulikuwa na kasoro fulani juu ya jambo hilo. Naam, bwana. Alijua kulikuwa na kitu fulani kibaya sana. Kwa nini? Hebu niwape. . . Maandiko hayalinukuu jambo hilo, lakini hiki hapa ninachopata. Ninajua ya kwamba—ya kwamba Yehoshafati alijua kwamba mnafiki huyo pale, Ahabu, ya kwamba yeye hakuwa sawa kwa Mungu. Naye Elija alikuwa ametabiri Neno la Mungu kwake. Basi Mungu angewezaje kubariki alichokuwa amelaani? Amina.

113 Ninasema jambo lile lile leo, rafiki. Nalo Kanisa la Mungu aliye hai, ambalo linadumu la kweli kwa Mungu, litasema jambo lile lile. Huwezi kuchanganya Mafuta na maji pamoja na kuita jambo hilo wokovu. Huwezi. Huna budi kujitenga, ndugu. Jambo fulani halina budi kutendeka. Kama kuna tumaini lo lote lililosalia, hatuna budi kufanya jambo fulani, na kulifanya upesi; kwa kuwa, ile saa, Kunyakuliwa kumekaribia.

114 Mambo yanalundikana, kila kitu, na kanisa liko mbali sana. Wao wanasoma kila aina ya magazeti, vitabu, hadithi, na kila kitu. Ningeenda leo kwenye. . . Ninaweza kwenda kwenye kanisa fulani, nami naweza kusema, "Loo, ni wangapi wanaojua. . . " Wao wanajua kila wimbo, baada ya moja ya fufuo hizi kuu. "Naam, wimbo *fulani* uko kwenye ukurasa ga—gani? Wao wanajua. Wanajua ni nani. Wanajua ni nani anayegombania Urais, na ni nani anayegombania *hiki*, na ni wachezaji wangapi mashuhuri wa sinema walifunga ndoa, *hili*, *lile*, na *linginelo*. Bali, Neno la Mungu, hawajui kitu juu yake. Naam basi. Kwa hiyo tunatoa ninino yao. . . Na, hata hivyo, wao wanakiri kuwa ni Wakristo.

115 Wala hao watu hawana hatia. Ni kutoka nyuma ya jukwaa, ndiko hayo yanatoka. Kweli kabisa. Ni kutoka nyuma ya jukwaa. Wao wanawafundisha kila namna ya mdundo, na kila namna ya *hiki* na *kile*, na madhehebu, jinsi ya kukufanya uhubiri, na kila kitu namna hiyo. Sijui kama jambo hilo limeleta manufaa? Sina kitu dhidi yake, lakini sijui kama hayo ni matakwa ya Mungu.

116 Wakati, Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hataingia katika ule Ufalme kamwe. Yeye atakayenifu-. . . atakayenifuata Mimi, na ajikane mwenyewe, na anasa zake za

kilimwengu, achukue msalaba wake anifuate Mimi." *Msalaba* ni mfano wa "mauti, maumivu." "Yeye atakayekuwa Mkristo, na ajivue mawazo yake mwenyewe. Na ajivue kazi zake mwenyewe. Na ajivue kila kitu, ajikane mwenyewe; kisha achukue msalaba ule uliowekwa wakfu, anifuate Mimi kila siku. Yeye atakayenifuata Mimi, na afanye jambo hilo." Hivyo ndivyo Yesu alivyosema.

117 Lakini, leo, tunasema, "Kila mtu awe na wakati mzuri. Kila mtu apige makofi. Kila mtu apige makelele, 'Haleluya!' Kila mtu afanye jambo *hili*." Loo, jinsi tulivyo na ghasia chungu zima! Amina. Mungu . . . Tunatoa nyimbo hizi mpya na kuziimba upesi sana, hata inaonekana kama kwamba tutapitia ukutani nazo, ama kitu kama hicho.

118 Wakati, nafikiri, kama tungekuwa tunaimba *Karibu Na Wewe, Mungu Wangu*, lingekuwa jambo bora zaidi kwa Kanisa; zile nyimbo za mtindo wa kale.

119 Kunaleta watu wengi wa taarabu ya dansi, mvulana fulani katika taarabu ya dansi hapa akicheza, jana usiku, na usiku huu hapa akicheza katika kanisa la Mungu aliye hai? Ni chukizo mbele za Mungu. Mtu huyo na athibitishwe, kwanza, na azae matunda, yanayopasa toba, kuonyesha ya kwamba yeye yuko sawa kwa Mungu.

120 Wanaleta ulimwengu wa jazz moja kwa moja jukwaani. Wanaleta mahubiri ya Hollywood, ya viinimacho, moja kwa moja jukwaani.

121 Mbona, hivi mimi sikukaa katika mji wenu mzuri, majuma machache yaliyopita, huko Louisville, Kentucky? Moyo wangu ulivunjika! Wakati hao wote walikuwa wameketi pale, wakiwa tayari kuona miujiza ya Mungu; na mara unapoihubiri Injili, wao wangejaa, kaktika sekunde moja, kisha wanakupa kisogo na kutoka nje ya jengo. Bila shaka. Hawaitaki Hiyo. Mioyo yao imefanywa migumu. Wanatoka nje; na wengi wao, Waprotestanti, pia, wanaohudhuria makanisa ya Kiprotestanti. Bali wao walikuwa wamejazwa . . . wamejazwa kabisa na viinimacho na kila kitu namna hiyo, upuzi na ukanisa, hata hawajui kitu juu ya Roho wa Mungu aliye hai. "Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake."

Ni siku ya namna gani tunayoishi! Angalia mahali jambo hilo linapolundikana.

122 Yehoshafati akasema, "Najua, Ahabu. Hao hapo wahubiri wako mia nne. Wao wote ni jamaa wenye sura nzuri, kila mmoja amevaa nguo na nywele zimechanwa vizuri, na kila kitu, cho chote kile wawezacho kuwa. Huenda wakawa na D.D.'s zao. Huenda wakawa na digrii zao za kila namna. Huenda wanajua Maandiko, kutoka A hata Z. Lakini hivi hauna mmoja zaidi, mahali fulani?" Na hapana mmoja tu zaidi, mahali fulani?

123 Yeye akasema, "Naam, kuna mmoja zaidi, lakini ninamchukia." Haya basi. Haya basi. "Ninamchukia." Kumbukeni, Ahabu alikuwa mtu wa kidini, na hawa walikuwa waalimu wa kidini, bali wao walimchukia mtu huyu aliyekuwa na Kweli. Kasema, "Ninamchukia." Kasema, "Yeye kila mara ananguruma jambo fulani dhidi yangu." Yeye angejizuiaje kufanya jambo hilo, wakati Neno la Mungu lilikuwa limemhukumu tayari?

124 Unawezaje kunyamaza kama wewe ni mtu wa Mungu, ama mwanamke wa Mungu, nawe unajua na kuona dhambi na kadhalika, zimelundikana na kupimwa, na kila kitu namna hiyo; na kuona nafsi za binadamu zikienda kuzimu, mamilioni kwa siku moja, halafu ukae kimya? Huwezi kufanya jambo hilo.

Mtu fulani aliniambia mimi hapa, "Unafikiri unaweza kukomesha jambo hilo?"

125 Nikasema, "La. Siwezi kulikomesha, maana Mungu alisema. Lakini siku moja, kwenye Kiti cha Hukumu, wao wataondoa lile pazia kubwa, wapige picha kule ng'ambo, na kanda iliyorekodiwa itachezwa. Nami nitasimama na kuisikiliza, nami nataka kusikia sauti yangu ikionya dhidi ya jambo hilo. Mungu atanihukumu wakati sauti yangu itakapokuja dhidi ya jambo hilo." Naam, bwana. Tunapoona maisha haya, kizazi hiki, vikichezwa tena kule kwenye Hukumu. Bila shaka. Tunaishi katika wakati mbaya sana. Huo hapo.

Nasi tunamwona; alisema, "Hivi hakuna mmoja zaidi?"

126 Yeye alisema, "Naam, lakini ninamchukia, kwa maana daima ananitabiria mabaya."

127 Anawezaje kujizuia kuhubiri mambo hayo magumu, wakati anayaona yakiendelea? Akimwona Ahabu akiishi jinsi alivyokuwa akiishi na kufanya jinsi alivyokuwa anafanya, na kuwaleta watu jinsi wanavyofanya!

128 Mtu wa Mungu, ama mwanamke wa Mungu, anawezaje kujizuia na kupiga makele na kukemea dhambi kutoka kila upande? Wakati, wanaona hawa wahubiri baridi, na wanaofanya viinimacho, na waalimu, na kadhalika namna hiyo, huko nje wakiwaacha watu waende jehanamu, kwa mamilioni, chini ya udanganyifu; wengi wa. . .hata watu wa utakatifu. Mimi sizungumzii sana juu ya Wamethodisti na Wabatisti, na mambo kama hayo; wao wanayo, pia. Lakini ni moja kwa moja miongoni mwao. Jamani!

129 Wakija jukwaani, wakiwa kama kitu kingine cho chote ila Wakristo, wakiishi kama kitu kingine cho chote, kila mahali nchini na kadhalika, halafu wanaiita "dini." Ni dini, lakini iko mbali sana na wokovu wa Bwana. Hiyo ni kweli. Wamewashika tu watu mpaka wamekuwa kundi tu la watu waliochochewa. Halafu mara maskini kuchochewa huko kunapokwisha, basi, muda si muda, huwezi kumpata mmoja wao; kanisa linabakia

tupu. Lakini kama mtu anampenda Mungu, yeye ataketi kwenye kiti chake kanisani, kila wakati. Hawezi kukaa nje. Hiyo ni kweli.

130 Sasa angalieni tu kwa dakika chache. Nitajaribu kuharakisha, kwenda moja kwa moja kwenye lengo sasa, maana wakati wangu unakwisha.

Angalia, kisha akasema, “Hivi hakuna mmoja zaidi?”

131 Akasema, “Naam, lakini ninamchukia. Yeye daima anatabiri dhidi yangu. Anasema mabaya juu yangu.”

“Vema,” kasema, “nenda kamlete.”

Akasema, “Jina lake ni Mikaya.”

132 Lakini mtu huyu alikuwa na dini ya kutosha kujua ya kwamba jamaa hawa hawakuwa sahihi.

133 Na mtu ye yote ambaye amewahi kuguswa, kidogo zaidi, na Roho wa Mungu, anajua ya kwamba mambo haya, kile kinachoitwa Ukristo leo, si kweli. “Huwezi kuupenda ulimwengu, wala mambo ya ulimwengu; kama ukifanya hivyo, kumpenda Mungu hakumo ndani yako.” Biblia ilisema hivyo.

Sasa angalieni. Alisema, “Nendeni mkamlete.” Nao wakaenda kule.

134 Ndipo yeye akamtuma maskini mjumbe mmoja, shemasi wa kanisa, labda, ama mtu fulani, akaondoka akaenda kule na kusema, “Sasa angalia, Mikaya, tutakuleta hapa mbele ya Ahabu na Yehoshafati. Sasa wote wawili wanaketi kule nje. Nao ni watu mashuhuri sasa. Wao ni walimu na ni wanachuoni. Nao wana digrii zao, na kadhalika. Na kila moja ya seminari zetu, kila moja ya makanisa yetu hapa, yamekubaliana kabisa ya kwamba haya ni mapenzi ya Bwana. Basi sasa wewe sema jambo lile lile wanalosema, na, ninakwambia, utavalia vizuri na kuendesha motokaa ya Kadilaki. Ninakwambia, utakuwa tu jamaa mashuhuri kama utafanya jambo hilo. Naam, bwana. Utafanikiwa.”

135 Mikaya akasema, “Kama aishivyo Bwana Mungu, nitasema tu neno lile anenalo Mungu.” Amina. Naam. Loo, huyo hapo mtu anayeupendeza moyo wangu. “Huenda ikanilazimu kula mkate na maji,” na alikula, “kwa ajili ya kufanya jambo hilo.” Huenda ukapigwa kofi la shavu moja na lingine, cho chote kile, lakini yeye alisema kweli na kuitetea. Mungu alilithibitisha kuwa kweli. Yeye hakuwa anapendwa sana na watu, bali alimjua Mungu.

136 Wakamleta maskini Mikaya pale. Akasema, “Haya, Mikaya, wasemaje juu ya jambo hilo?”

137 Akasema, “Kweeni. Kweeni.” Kasema, “Kweeni, katika amani. Nendeni, mkafanikiwe, hivyo ndivyo ninawataka mfanye. Lakini niliwaona Waisraeli kama kondoo, bila

mchungaji, kilimani, wametawanyika. Jambo ndilo hilo," akasema.

138 Basi hapo alipofanya hivyo; ndipo Ahabu akageuka, na Yehoshafati. Kasema, "Nilikwambiaje? Mtakatifu huyo anayejifingirisha, ama cho chote kile," samahani, "ama cho chote alichokuwa, jamaa huyo alisema jambo hilo! Nilikwambia nini? Jamaa huyo angebashiri mabaya tu, mabaya juu yangu. Nilikwambiaje? Yeye angehukumu tu kanisa letu, na kuhukumu wahudumu wetu, na kuhukumu utaratibu wa dini yetu. Nilikwambiaje? Yeye angesema jambo hilo. Ninamjua. Nilimjua babaye kabla yake." Amina. [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] "Nilijua baba yake kabla yake." A-ha, naam, bwana, mtu halisi wa Mungu. Kasema, "Nilijua angesema hivyo."

139 Na kwa hiyo akasema, "Naam," kasema, "Niliwaona Waisraeli kama kondoo, wametawanyika, bila mchungaji, kilimani." Halafu basi akasema, "Mimi . . . "

140 Kisha mmoja wa jamaa hao aliyekuwa na pembe kubwa, alikuwa akitaka kusukuma. Mhubiri fulani akaja akamvuta na kumgeuza Mikaya, akampiga kofi mdomoni kwa nguvu alivyoweza, kasema, "Alitokaje Roho ya Mungu alipotoka kwangu? Kama unajua."

141 Kasema, yeye akasema, "Ngoja mpaka utakapokuwa umeketi gerezani hapa, utajua alitokaje." Hiyo ni kweli.

142 Ngojeni mpaka Urusi inaketi hapa nje, imeteka mataifa na mambo kama hayo, na nchi hii, kwa sababu ya kurudi nyuma kwake, nanyi mtaona kilichokuwa kweli na uongo. Hiyo ni kweli. Mtaona kama dini yenu yenye uvuguvugu itakuwa na faida yo yote, ama la.

143 Hebu taifa hili lilie, si kucheka na kuigiza. Hebu taifa hili liende magotini, katika toba. Hilo ndilo tunalohitaji. Si ufufuo wa kuwaingiza watu wengi sana kanisani. Tunapaswa kufunga kila klabu cha pombe, kukomesha kuvuta sigara kote, kuvuja hivyo viwanda. Kuanza kampeni halisi ya mtindo wa kale ya Roho Mtakatifu; ambapo wanaume kwa wanawake, mchana na usiku, wakilala kifudifudi, wakilia. Nitawaambia, itakuwa ni kinga kubwa sana taifa hili lililowahi kupata. Hiyo ni kweli.

144 Hebu Maskani ya Branham iache upuzi wake. Hebu irudi hapa nyuma madhabahuni na ijiweke sawa na Mungu. Isahihishe mambo na majirani, na kadhalika namna hiyo, ndipo iwe sawa na Mungu. Hamtakuwa na mizozo yo yote na mambo yasiyofaa; itakuwa mahali pa kuvutia ulimwenguni. Hiyo ni kweli. Naam, hiyo ni kweli.

145 Kisha akasema, "Roho wa Mungu alitokaje, kutoka kwangu?"

146 Mikaya akasema, "Nilimwona Mungu na jeshi Lake, baraza lake, ameketi Utukufuni."

147 Mnajua, Mungu hufanya baraza kule Juu, mara kwa mara. Yeye, Yeye huwaleta ninino Wake—Viumbe Vyake Malaika na kufanya ba—baraza, mara kwa mara, huko Mbinguni.

148 Kisha akasema, "Nilimwona Yeye ameketi katika Kiti cha Enzi, na watu wote walikuwa wameketi mkono Wake wa kulia na wa kushoto." Tena akasema, "Wao walikuwa wanajadiliana, 'Ni nani tunayeweza kumpata ashuke aende akamdanganye Ahabu, akamlete hapa nje akatimize unabii wa Eliya? Mungu tayari amesema jambo hilo, kile kingetukia, kwa hiyo tutaona tu ni nani anayeweza kushuka aende.'

149 "Ndipo pepo wa uongo akatoka kutoka pande za chini," bila shaka, kutoka kuzimu, "akaja mbele za Mungu akasema, 'Nitashuka niende kule, niwaingie wahubiri wale na kuwafanya hao wote kutabiri uongo.'" Loo, hivi hao hawakukasirika! Je! jambo hilo liliwafanya wajisikie vinginevyo, wakati waliposema, nitashuka niende niwafanye hao wahubiri, kila mmoja wao, kutabiri uongo.'" Ndipo akashuka akawaingia wahubiri hao, nao wakaanza kutabiri uongo.

150 Basi, ewe ndugu, Mungu yule yule anatawala kwenye Kiti cha Enzi kile kile leo. Na pepo yule yule wa uongo amefanya jambo lile lile leo, kutabiri uongo.

151 Wao waliendelea kusema, "Amani, amani, amani," baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia.

152 Hebu niwaonyeshe mahali ilipotoka. Katika Vita vya Kwanza vya Dunia, wakati Ufaransa kule ilimwacha Mungu, katika ufisadi wao wa miaka ya '90, kisha wakaanza . . .

153 Sasa nitaingilia kidogo mambo ya maadili, kwa hiyo nyote ketini kimya kabisa kwa dakika chache.

154 Angalieni, kule nyuma, hapo mwanzo, kule Ufaransa, huko ndiko hamaki na uchafu ulikoanza. Kama kuliwahi kuwa na shimo la upotovu ulimwenguni, ni Paris, Ufaransa. Nami karibu nimeizunguka karibu yote, na hapo ndipo mahali pabaya sana nilipowahi kuona. Pia London, Uingereza si tofauti sana. Nayo Marekani imeanza kufuata nyayo zake. Hiyo ni kweli. Hao hapo.

155 Kila unapoharibu uadilifu wa tabia za wanawake, unavuja uti wa mgongo wa taifa.

156 Hapa unaenda kule, katika nchi zao wenyewe, na kusema wewe ni mmishenari, wao hawataki . . . Kasema, "Mtatwambia tufanye nini, jinsi ya kuimba nyimbo chafu kuhusu wake zetu, ama kuhusu wasichana wetu? Mtatwambia jinsi ya kuwataliki wake zetu? Mtufundishe kunywa wiski na kufuata nyayo zetu?" Hivyo ndivyo tulivyo sisi.

157 Tunaweza kujiita taifa la kidini, taifa la Kikristo. Vema, hao "makafiri" kule Afrika wangeweza kutufundisha uadilifu,

namna ya kuishi. Mahali palipooza sana, katika Marekani, ama karibu ulimwenguni, ni taifa hili, jinsi limefikia. Mimi ni Mmarekani, bila shaka. Lakini, ndugu, siwezi kujisaidia . . .?. . . mbele ya Ahabu ama Yehoshafati, nami sina budi kusema yale Mungu asemayo ni Kweli. Hilo ndilo jambo ambalo kanisa linahitaji kutetea, leo. Kama ikifikia kati ya taifa na Mungu, ni Mungu, daima. Naam, bwana.

158 Angalia, katika Ufaransa, wao walianzisha upuzi wao wote, na kuendelea jinsi waliovyoishi kule. Ndipo Mungu akawatumia Ujerumani, kuwatwanga kidogo. Ndipo tukaondoka tukaenda kule kuwaokoa. Na mara tulipofanya hivyo, na kushinda vita, tukawafukuza Wajerumani, tukafanya amani na Ufaransa, je! wao walimgeukia Mungu? La, bwana. Wanawake, divai, ulevi, dhambi na uchafu mtupu!

159 Ndipo wakafanya nini? Nini kilichotendeka? Hapa ndipo tulipoanza. Ibilisi alifanya makao yake makuu kule. Huko ndiko alikoanza, huko huko, kuuharibu ulimwengu, kutoka Paris, Ufaransa.

160 Halafu, kama mkiangalia, yeye asingeingia hapa kupitia kwenye huduma, kwa hiyo jambo alilofanya lilikuwa ni kuhamia Hollywood hapa nje. Yeye alianzisha Holl-. . . Alihamisha makao yake makuu hapa Hollywood. Ibilisi alishuka hapa nyuma, miaka michache iliyopita, miaka kumi na mitano ama ishirini iliyopita, akiwa na jeshi lake kuu, akaenda, akaivamia Hollywood, California. Naye ameivamia Marekani pamoja na nguvu zake za kipepo. Kweli! Mitindo yetu yote inatoka Paris. Inaingia Hollywood, mpaka kwenye sinema. Wasichana hawa wadogo na wavulana wadogo, na kadhalika, wanatoka nje hapa, wanaangalia michezo hiyo ya sinema.

161 Watoto wadogo wazuri, jamaa wadogo wazuri, sina kitu dhidi yao. Mungu na aibariki maskini mioyo yao! Moyo wangu unawaonea uchungu sana.

162 Na papa hapa mjini, nilikuwa nikizungumza na nini hii yangu. . . mmoja wa. . . Mvulana wangu, juzijuzi, alisema, "Baba, laiti kungalikuwa na wavulana hapa karibu, mjini, waliokuwa na Roho Mtakatifu, na kadhalika!" Mnashangaa kwa nini nilikuwa nikienda Denver, Colorado, ama mahali pengine kama hapo? Kuwapeleka watoto wangu mahali fulani ambako kuna kundi la watu wanaomlilia Mungu! Ndicho tunachohitaji, ndugu!

163 Nchi hii, taifa hili, mji huu, mahali hapa, pameharibika sana hata ni jambo la kuhuzunisha. Laiti ningaliweza kueleza sasa hivi yale ninayojua kabisa kwamba ni kweli papa hapa, lisingekuwa jambo la kuelezwa mbele ya kusanyiko lililochanganyikana. Ama, papa hapa katika mji huu papa hapa; si hapa tu, bali mahali pengine, kila mahali, mambo yameanza kuwa tu. . .

164 Kwa sababu gani? Watu. . .Angalieni, marafiki, amekuwa mjanja sana. Ameingia kwa urahisi sana, hata anakukaba koo. Ibilisi alikuwa katika mitindo. Huenda hajaishiwa na mitindo, bali hajaacha biashara yake, nitawaambia jambo hilo. Yungali biasharani.

165 Angalieni, leo. Tunachukua, kama nilivyosema muda kidogo uliopita, juu ya maskini bibi fulani, maskini msichana mdogo mwenye waridi. Kwa mfano, hilo waridi, linapendeza; liko pale lipate kuangaliwa, hiyo ni kweli. Na hiyo ni kama tu kanisa, liko pale lipate kuangaliwa. Kama maskini mwanamke mrembo, yuko pale kutanzamwa. Hiyo ni kweli. Lakini kama yeye . . . Yeye ni mzuri, kwamba yuko hivyo kwa mumewe, yeye—yeye ni sawa. Bali kama hana upanga wa uadilifu uliochomoka pale kumlinda, yeye anakuwa aibu kwa uma na kwa binadamu; anakuwa duni sana na wa kuaibisha na ameoza hata mbwa wasingemwangalia. Hiyo ni kweli.

166 Na jambo lile lile kwa kanisa la Mungu aliye hai! Wao wanatoka hapa nje na kujaribu kufanya viinimacho na kujitengeneza, na kutenda kama . . . Wanawavua wanawake wao nguo hapa, moja kwa moja . . . nao watu hawatambui ya kwamba pepo hawa wanazivamia nyumba zenu.

167 Papa hapa kwenye ujirani wangu juzijuzi, bibi mdogo ambaye nafikiri ni mwanamke mzuri . . . Naye ni mwanamke aliyeolewa, ana mtoto. Ndipo maskini mwanamke yule akatoka kule nje. Mwanamume fulani alishuka akaja barabarani kufanya kazi fulani, naye mwanamke huyu akatoka huko nje amevalia nguo hizo fupi sana, lilikuwa jambo la kuchukiza.

168 Haya ni mazungumzo mabaya sana ya Sikukuu ya Mama. Lakini, ndugu yangu, hebu nikwambie kitu fulani. Mama, rudi ukafanyike mama tena!

169 Hata kwa maskini kijivulana kidogo kilichokuwa kinazuru karibu na kwetu, kiliingia kikatuambia juu ya jambo hilo, "Angalieni kule!"

Nikasema, "Vema, hilo si kitu."

170 Huyo mwanamke ni mwanamke mzuri. Sisemi yeye hana uadilifu. Lakini, jambo ni kwamba, kuna roho ya hamaki, chafu iliyo juu yake, ikimfanya afanye jambo hilo, wala hajui.

171 Mama angetaka kitu gani ulimwenguni, ama mtu ye yote, kuvaa maskini nguo hizo fupi na chafu, na kujianika wenyewe mbele ya mwanamume? Wewe ni mrembo, dada. Wewe ni mrembo, mama. Namshukuru Mungu kwa ajili yako. Lakini, wewe ni mrembo, bali huna Roho Mtakatifu pale kulinda uadilifu huo. Afadhali kama ungalikuwa na sura mbaya sana hakuna mtu angekuangalia, halafu ukaenda Mbinguni. Hiyo ni sawa. Hiyo ni kweli. Angalia yale unayofanya; huo uadilifu.

172 Naam, jambo ni kwamba, Ibilisi ameingia na amewaambia watu mambo haya. Ameingia ndani ya wahubiri; anajifananisha na Hollywood. Wasichana na nini hii wadogo—mabibi wadogo, wao wanajifananisha na Hollywood. Vitu bora zaidi walivyo navyo nchini leo, uadilifu wa kupindukia unaoweza kusikia, ni kuzungumza kuhusu mazungumzo ya redio.

173 Maskini mwanamke mzee kama Bi Kay Star, sina kitu dhidi yake; bali kumwona mwanamke mzee, mwenye umri wa miaka hamsini, na kadhalika, huku nguo zake zote zimembana sana, kana kwamba alikuwa amemiminwa katika gunia la mahindi. Sisemi jambo hilo kwa mzaha, maana ninazungumza dhidi ya mambo hayo. Bali mwanamke anayetenda jambo kama hilo, na kusimama na kuwa mfano wa vijana wanawake wa Kimarekani, ni aibu kwa taifa letu. [Ndugu Branham anagongagonga mimbara mara tano—Mh.] Ni Ibilisi.

174 Jamaa kama Arthur Godfrey na hao wengine wakikimbia kila mahali hapa, wakifanya mambo wanayofanya, na mtu anayejulikana sana nchini namna hiyo, naam, mbona, ni aibu.

175 Haleluya! Ninasema jambo hilo kwa sababu nahisi Roho Mtakatifu yuko hapa. Kuvamiwa kunaendelea, kukifagia nyumba baada ya nyumba, mahali baada ya mahali, kanisa baada ya kanisa, toka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine.

176 Enyi watoto, katika Jina la Yesu Kristo, simameni katika msimamo wa ufufuo na Bwana Yesu Kristo, na kusema, "Nitashika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa." Naam, bwana. "Nitakuwa mama halisi." "Nitakuwa baba halisi."

> Wakati ulimwengu wote, na yote yaliyo karibu,
> yote yaliyo karibu na nafsi yangu yakiisha,
> Basi Yeye ndiye tumaini langu na nanga yangu.
>
> Kwake Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama;
> Mahali pengine pote ni mchanga unaodidimia,
> Mahali pengine pote!

177 Ni kitu gani kilisababisha upuzi huu wote? Ni nini kilichosababisha wahudumu kutenda jambo hili? Ni kitu gani kilichowafanya wahubiri kuwatabiria watu uongo huu?

178 Mbona basi, miaka kadha iliyopita, ninyi Wamethodisti . . . Wakati mzee John Smith alipochukuliwa akapelekwa kwenye mimbara yake, kuhubiri Injili, naye akahubiri mahubiri mafupi ya masaa manne. Ndipo akasema, "Shida yake ni kwamba, moyo wangu unavunjika." Akasema, "Binti wa Kimethodisti hata wanavaa pete vindoleni mwao."

179 Naam, siku hizi, wanavaa kaptura na maskini nguo chafu fupi. Nao watakuwa uchi kabisa, katika miaka mingine mitano, jambo fulani lisipotendeka. [Ndugu Branham anagongagonga

mimbarani mara tatu—Mh.] Ni kitu gani kilichowapata enyi Wahubiri wa Kimethodisti, enyi Wakampbeli, enyi Wabatisti? Naam, bwana. Ni Ibilisi, ameshusha nguvu zake, naye ana vishetani vyake hapa nje.

180 Wala hamtambui jambo hilo, ninyi mnaovuta sigara, enyi wanawake, huku mkifanya jambo mnalofanya huko nje, huku mkinywa pombe na kufanya yasiyofaa jinsi mnavyofanya. Hamtambui kwamba mnatia sumu mwili wenu, na kuangamiza vizazi vyote vitakavyowafuata, kama kuna kitu kama hicho. Nafasi asilimia themanini na tano zaidi ya kuambukizwa na kansa, kwa kuvuta sigara, nanyi mnaingilia mambo hayo makusudi. Nayo makanisa yanaunga jambo hilo mkono.

181 Katika kanisa kubwa la Kibatisti hapa, hivi majuzi. Ninakemea Mbatisti. Nina haki ya kufanya jambo hilo; wao kwa namna fulani wanaegemea upande ninaotoka. Bali ilipowabidi kutoa nafasi kati ya ibada ya shule ya Jumapili na ibada ya mahubiri, ili kwamba mchungaji na hao wengine wote wapate kutoka nje na kuvuta sigara, na barabara ilijaa wanaume na wanawake wanaovuta sigara. Ibilisi amefanya jambo hilo. Hiyo ni kweli.

182 Halafu, hapa katika mji wetu wenyewe, mmoja wa wahudumu wetu mashuhuri sana, papa hapa katika New Albany, kwenye uwanja huu wa michezo, ati mmoja wa wahudumu wetu mashuhuri mjini anaongoza kipindi cha dansi ya mraba, apate kuwaleta wanaume na wanawake jukwaani.

183 Sijali ulimwengu unasema nini, sijali jinsi unavyojaribu kubembeleza kwenye jambo hilo; ndugu, hakuna mwanamume mwenye damu nyekundu anayemvuta mke wa mwanamume mwingine, na kujisikia sawa. Unajua jambo hilo ni kweli.

184 Wao wamewachukua wanawake wetu, wakawavua nguo; kule nje maofisini, na kuendesha teksi, na huku na huko mitaani. Ambapo, wao wanapaswa kuwako nyumbani, nyuma ya jiko, wakipika, wakitayarisha vyakula.

185 Ni kitu gani? Ni Ibilisi. Kuvamiwa kunaendelea. Mimi sisemi kitu juu ya mtu *huyu* binafsi wala mtu *yule* binafsi. Ninasema ni pepo wachafu wanaowapagaa watu, wakiwaingiza moja kwa moja katika kitu hicho. Kuvamiwa kwa Marekani!

186 Kupinduliwa kwa kanisa! Kanisa limepinduliwa na Ibilisi. Kule nyuma . . .

187 Wao wanamchukua mvulana sasa, anapokuja kwenye seminari, jambo la kwanza analopaswa kujifunza ni kupata digrii zake. Hana budi kujifunza saikolojia. Hana budi kujifunza theolojia. Hana budi kufundisha, afundishwe upuzi wa kila namna. Kama hana elimu bora kabisa, kama yeye si mwerevu na mwenye akili awezavyo kuwa, basi wao watamfukuza; hawezi kufaulu. Yeye atafanyaje? Kwa hiyo, anatoka anaenda hapa na kutoa hotuba ndogo ya kisiasa, tuseme, hotuba ya kisiasa ya

kanisa, kwa kundi la watu, kundi la wanaume na wanawake wanaokufa.

188 Ee Mungu, tutumie watu wa mtindo wa kale na wagumu, wasiojua tofauti ya A na B, wanaojua Nguvu za ufufuo wa Bwana Yesu Kristo, ambao watahubiri toba, na kuwapeleka wanaume na wanawake madhabahuni, wapate kumpenda Bwana Yesu. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]

189 Ni aibu. Yeye amezivamia seminari. Ameyavamia makanisa. Amewavua wanawake wetu nguo. Amewafikisha wanaume wetu mahali ambapo usingeweza kuwaambia jambo lo lote. Na, wanaume na wanawake, nafikiri . . .

190 Mnasema, "Vema, hao wanawake!" Naam, nanyi wanaume mnaowaruhusu wake zenu kufanya jambo hilo, jambo hilo linaonyesha mmefanyiziwa kutokana na kitu gani. Hiyo ni kweli kabisa. Bila shaka. Ni fedheha. Msiba kweli.

191 Kisha moja kwa moja mpaka kwa mhubiri. Mhubiri husimama jukwaani, leo, la mi- . . . mimbara ya kisasa. Anasimama hapo ndani, huku watu wake wako mbele yake, na kuhubiri kila kitu kidogo ulimwenguni mbali na toba na dhambi, na msalaba wa Kristo unaoparuza. Naam.

192 Unapoyaweka mambo jinsi yalivyo; watu wanakuja kukusikia, katika ibada ya kiinjilisti. Unajaribu kupata hilo jambo na kuihubiri Injili, na kuwafanya watu watubu na kuwatoa nje; wao watashikwa na hamaki na kutoka nje, wao, "Si lazima tusikilize jambo Hilo." La, wao si lazima walisikilize. Lakini, ndugu, itawabidi kutubu la sivyo wataangamia.

193 Pepo! Unaenda shuleni; wamezivamia shule. Angalieni kila mahali, kila mahali nchini leo. Angalieni hapa, enyi watu, enyi Waprotestanti. Angalieni, kuna shule nne kubwa mno za Kikatoliki na kadhalika, zilizojengwa leo. Ni kwa nini? Mnaachilia milango.

194 Sina kitu dhidi ya Ukaotoliki, ingawa siuamini. Mimi ni Mprotestanti hasa. Hiyo ni kweli kabisa, naweza kuthibitisha ya kwamba wao hawanini hii . . . Usingeweza kubishana nao. Wao wanasema, "Hatujali Biblia inasema nini. Tunajua yale kanisa lisemayo."

195 Mungu yumo katika Neno Lake. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara tano—Mh.] Hapa ndipo alipo Mungu.

196 Lakini baadhi ya Wakatoliki, wakishika kanisa lao, wangekufanya ujionee aibu, kama Mprotestanti. Laiti ungeweza kuishika Biblia, jinsi wanavyolishika kanisa! Hiyo ni kweli. Lakini, wao wamekosea. Ninaweza kusema jambo hilo chini ya mamlaka ya Mwenyezi Mungu, ya kwamba, wao wamekosea. Kabisa.

197 Nanyi Waprotestanti mmekosea, jinsi mnavyofanya, maana kweli mnajua vyema zaidi, na mnafanya hivyo. Jambo hilo

linawafanya wanafiki. Hakika, ni kuvamiwa; makanisa yanaachilia. Na sasa badala . . .

198 Kanisa, kujaribu kulifanya kanisa liwe zuri, kujenga kanisa kubwa zaidi, kuweka minara mirefu juu yake, vinanda vikubwa mno vyenye mabomba, na kufanya kila kitu kujaribu kujifananisha na kanisa Katoliki. [Ndugu Branham angonga mimbarani mara kadha—Mh.] Hamtaki kujifananisha na kanisa Katoliki, kama limewekewa kwenda kwenye maangamizi. Kwa kuwa, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI, limepasiwa kwenda katika maangamizi. Nanyi mkijifananisha nalo, mtaambatana nalo.

199 Lakini tonachohitaji leo si kanisa kubwa, mnara mkubwa; ni madhabahu za mtindo wa kale ambapo dhambi zinateketezwa, chini ya maombi ya wanaume na wanawake wanaompenda Bwana Yesu Kristo. Mnajua jambo hilo. Hayo ndiyo tunayohitaji. Nisikilizeni, enyi marafiki. Nisikilizeni. Ni upendo.

200 Wakati wangu umekwisha. Ningetaka tu kukaa kidogo juu ya jambo hilo, ambapo . . . Nitaendelea nao, baadaye kidogo, kuvamiwa huko, mahali kulipoelekea. Amevamiwa. Ameyavamia mataifa yetu. Ameivamia Marekani.

201 Sasa kumbukeni, mimi sijawahi kupiga kura maishani mwangu; mnaona, nikasema . . . kujivunia. Hizo ni haki zangu za Kimarekani kama nikitaka kufanya hivyo. Bali ninawathamini sana rafiki zangu, kuwaweka mle. Angalieni, nimewaona wakiingia mle kama watu wazuri, wakatoka kama majambazi, nami sitaki jambo hilo.

202 Nina jambo moja. Niko mahali hapa nikijenga jukwaa kwa ajili ya Mtu Mmoja ambaye ndiye mgombea uchaguzi, na huyo ni Yesu Kristo, na Huyo pekee. Ninatoa wakati wangu kwa ajili Yake. Hiyo ni kweli. Kama naweza kulinyosha kanisa, ulimwengu uliosalia utajishughulikia. Hiyo ni kweli.

203 Bali hebu niwaambie, wakati Bw. Roosevelt . . . Huyo mtu amekufa. Namtakia heri; natumaini yu heri. Alipoingia, akaendelea kwa vipindi vitatu vinne, naye akatawala, utangulizi tu wa utawala wa mabavu. Ninaweza kuwathibitishia jambo hilo katika Maandiko, ambapo Hayo yalisema jambo hilo lingetukia. Hiyo ni kweli. Hatuna katiba ya nchi tena. Imevunjwa-vunjwa vipande-vipande. Kila kitu kimevurugika. Warepublican ni wabaya vivyo hivyo. Ni sita upande mmoja, na nusu dazani upande mwingine.

204 Kwa kuwa, kila ufalme utapondwa-pondwa, bali Ufalme wa Yesu Kristo utasimama na kutawala milele. Hiyo ni kweli. Juu ya . . . Danieli aliona Jiwe lililokatwa milimani, likaupiga ulimwengu wa kisiasa kule nyuma likauponda-ponda ukawa poda iliyosagwa namna hiyo, kama ngano katika sakafu ya kupuria katika majira ya kiangazi. Lakini Jiwe hilo

lilikua likawa mlima mkubwa sana ambao ulitandaa hata juu mbingu-. . . ukaijaza mbingu yote na nchi. Hivyo ndivyo ilivyo.

205 Ulimwengu wa kisiasa umekwisha. Taifa letu limefilisika. Ninyi kumbukeni jambo hilo, ya kwamba Ndugu Branham alisema jambo hilo, BWANA ASEMA HIVI. Taifa letu limeangamia. Halitainuka kamwe. Limekwisha, kama mataifa mengine yote. Ndilo taifa lililo kuu sana ulimwenguni, linalosimama leo, bali mbegu halisi ya Ibilisi imepandwa tayari katika mioyo ya hao watu; jinsi ilivyoingia huko Hollywood, jinsi ilivyotoka ikaingia ndani ya watu, wakaanza kufanya jambo hili. Nawe huwezi kuwaambia kitu cho chote.

206 Mwekeni Rais kule atakayejaribu kufunga wiski, wala asikataze, mwone litakalotukia. Atapigwa risasi, masaa mawili baada ya kuingia mle. Hakika, hawezi kuvumilia jambo hilo; ulimwengu mzima unamchukia. Naam, bwana. Usingeweza kufanya jambo hilo.

207 Limekwisha. Limevamiwa, nayo roho ya ukomunisti imetwaa mamlaka.

208 Nenda kwenye mashule yetu leo, angalia watoto wetu wa shule. Maskini watoto wetu wanaokwenda shuleni, mnapaswa tu kujua yale yanayoendelea. Maskini wasichana wadogo hapa shuleni, na vitu kama hivyo, kwenye umri wa miaka kumi na minne na kumi na mitano, mama zao waliwapeleka shuleni, wameharibiwa kimaadili, kiakili, mashetani wa madawa ya kulevya, wamezoea madawa ya kulevya, wavuta sigara kwa fujo, kila kitu kingine namna hiyo; na wenye umri mdogo sana, watoto wadogo namna hiyo. Ingekuwa vigumu kumpata bikira kati yao kama ilivyo kupata sindano kwenye lundo kubwa la ukoka mkavu, mahali wana miadi ya blanketi na vijana, na kujilaza katika kingo hizi za mto na po pote pale.

209 Nami ninaweza kuwathibitishieni, enyi rafiki zangu. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara tatu—Mh.] Nisingesema jambo hilo mimbarani isipokuwa nilijua nilichokuwa nikizungumzia. Kuhusu shule papa hapa katika wilaya ze—zetu, papa hapa katika wilaya hizi, juu ya kuvalia kwa maskini mabibi hao wadogo, hawajui. . . wakiwaambia mama zao ya kwamba wanakwenda mahali mbalimbali, huku wanakutana na vijana na hata kufanya umalaya kwenye mitaa ya Louisville, (ni kitu gani?) na kuimba kwenye kwaya.

210 Kwa sababu, wao wana maskini Injili ndogo ya urafiki inayodumu pale, ambapo wahubiri wanasimama na kuzungumza juu ya mambo madogo yasiyo na maana, na vijihadithi vidogo vya Biblia, ama kitu kama hicho, badala ya kuhubiri toba na kuwaleta wanaume na wanawake madhabahuni.

211 Baba yake anaingia usiku na kuwasha msokoto wake, anachukua glasi ya pombe, anaketi chini na kuinywa. Mama

hayuko, mchana kutwa, akiwa pamoja na kundi la wanawake kwenye karamu ya kadi, mazungumzo ya urafiki kama hayo. Mnawezaje kumtarajia huyo mtoto kuwa kitu kingine cho chote?

212 Angalieni, haidhuru unaishi katika mazingara gani, hivyo ndivyo ulivyo.

213 Hebu mchukue maskini msichana mdogo, maskini mvulana mdogo, waweke nje huku, waache wakae na mtu fulani. Hebu mchukue mwanamume, ninaweza kumchukua mvulana wangu, nimwache awe huko nje na mtu fulani; ngoja nirudi, daima ninaweza kukwambia amekuwa na mtu gani. Bila shaka. Angalia, mazingira hayo, roho huyo anamshika.

214 Hebu ingia kanisani, mahali ambapo watu wote. . .hebu uingie kwenye makanisa ya Roho Mtakatifu, ama makanisa ya kipentekoste, wanavyoyaita. Hebu kila mtu awe. . .Loo, wao wanakimbia na kutikisa kichwa chao huku na huko, mchungaji anafanya hivyo; angalia kanisa lote likianza kufanya jambo lile lile. Hebu mwanamume, hao watu, waamke na—na kufanya tu mambo ya kuchukiza, ama cho chote kile; angalia kitu hicho chote kikifanya jambo hilo. Ingia mahali ambapo mchungaji ni mkavu kweli kweli na baridi; angalia kundi lote likifanya jambo hilo. Unaingia katika mazingira hayo.

215 Mchukue mwanamume ambaye ni mtu mzuri na mwadilifu, acha amwoe maskini mwanamke mdogo asiyefaa hata kwa thamani ya hela moja; haichukui muda hata mwanamume huyo akawa hafai kwa thamani ya hela moja pia. Hicho ndicho kilichompata Ahabu. Basi chukua jambo Hilo hilo vinginevyo, acha maskini mwanamke mzuri amwoe maskini mwanamume asiyefaa kwa thamani ya hela moja; muda si muda, mwanamke huyo anafanya jambo lile lile analofanya mwanamume yule.

216 Jinsi ningeendelea, asubuhi hii, na kuelekeza mikono yangu kwenye maskini nyumba zilizovunjika na mambo kama hayo, ambapo maskini mama wazuri huingia kwa baba mlevi, na mambo kama hayo, wakadhania wangeweza kuwasaidia, na sasa mama mzima na wengine wote wanakunywa na kuendelea. Ni mazingira.

217 Ni kitu gani? Ni Ibilisi. Ni Ibilisi, kule kuvamiwa. Yeye aliingia mbio katika taifa hili, kama simba angurumaye. Akaketi chini hapa katika mahali pazuri sana walipokuwa napo, katika Hollywood. Akasema, "Ninaweza kuleta sinema hapa mpaka televisheni zitakapokuja, kisha nitawapata." Ndipo akaketi chini huko.

218 Nao watu wa kanisa, badala ya kufunga sinema hizo na kuwakataza watoto wao kwenda, wao wanawapa senti kumi Jumapili alasiri na kuwapeleka huko, ili kwamba wapate kuwa na karamu ndogo ya kadi ya kustarehe pamoja, wawe kule nje peke yao na kuzurura kila mahali. Loo, ni fedheha jinsi gani! Sasa wao wanafungulia tu televisheni na kuangalia upuzi wote

mchafu, uliooza ulioko ulimwenguni, kwenye kitu hicho. Hiyo ni kweli.

219 Mimi sina kitu juu ya sinema. Sina kitu dhidi ya televisheni. Ni huo upuzi uliooza ulimo mle. Hivyo ndivyo ilivyo. Kama mngaliiweka adilifu, ingalidumu na uadilifu.

220 Usingeweza kuuza viatu vya mtindo wa kale vya vifungo hapa mjini, leo, kamwe. Wanawake hawavitaki. Wao wanataka vidole vijitokeze nje ya viatu. Wanawake wengine wanafanya jambo hilo. Hiyo ni kweli.

221 Ukienda kanisani, huwezi kuwauzia ile dini ya mtindo wa kale, maana, huyo mwanamke mwingine, hataki uhusiano wo wote na jambo hilo. La, bwana. "Sijui sababu ya kushuka kwenda kule. Ninaamini tu, hakuna lingine." Loo, ndugu, Ibilisi anaamini, pia. Hiyo ni kweli. Utatubu la sivyo utaangamia.

222 Naam, samahani; la, sivyo. La, sivyo. La, ninaghairi jambo hilo. Ninawapenda watu. Lakini ni—ninawapenda sana hata nisingetaka kuwaona mkitumbukia kichwa mbele namna hiyo. Mungu akipenda, nitaendelea na jambo hili baadaye kidogo juma hili.

223 Naam, kwenu ninyi mama ambao ni mama, neno moja tu kwenu kabla hatujaondoka. Mungu awabariki. Waleeni watoto wenu iwapasavyo.

224 Tutaendelea na kuvamiwa kule; hatuna budi kwenda majumbani bado, na mahali mbalimbali, shule, na huko nje mahali mahali na jambo hili. Tutaendelea nalo.

225 Lakini, kule kuvamiwa kwa Marekani, Ibilisi ametwaa mamlaka juu yake. Msiogope Urusi. Urusi haina la kufanya. Tunafanya jambo hilo sisi wenyewe, upotovu wetu wenyewe moja kwa moja kati yetu. Hiyo ni kweli.

226 Mwajua, Marekani ina visa vingi vya talaka kuliko ulimwengu wote; talaka nyingi zaidi. Wazia jambo hilo. Hilo linatisha sana? Umama umevunjwa tayari. Mama hawakai tena nyumbani pamoja na watoto wao, kama walivyokuwa wanafanya. Hawana budi kuajiriwa.

227 Hapa hivi majuzi, mwenye duka fulani humu mjini, alikuwa ananielezea jambo hilo. Wanawake hawa wanaofanya kazi katika viwanda hivi vya umma, wanawake hawa wachanga walioolewa na wana watoto wadogo kadha. Wana yaya wanaowalea watoto wao. Wao wanafanya kazi katika viwanda hivi vya umma. Kasema, "Kulikuwako na wawili wao wamesimama pale, . . .? . . . waliofukuzwa kazi, kwenye kazi zao za umma, kasema, 'Usijali. Tutafaulu, haidhuru.'"

228 Loo, ni saa ya umalaya jinsi gani iliyowadia! Hakika. Ibilisi tayari amewaambia ya kwamba wao ndio mabosi nyumbani. Wao watakuwa na njia yao wenyewe. Watafanya wanalotaka

kufanya. Nawe jaribu kuondoa jambo hilo ndani yao, kama unaweza.

229 Kuna kitu kimoja pekee kinachoweza kutoa jambo hilo ndani yao, nacho ni madhabahu, mbele ya Yesu Kristo, dini ya mtindo wa kale, yenye kijito cha majonzi itakayoivunja mioyo yao na kuwararua vipande-vipande, na kuwafanya wanachohitajiwa kuwa. Hiyo ni kweli.

230 Wao wanaweza kuwazia ya kwamba mimi ni mzee wa mtindo wa kale. Lakini siku utakayokuwa unakufa, ndugu yangu, dada, utatambua ya kwamba nilikwambia yaliyo Kweli. Hiyo ni kweli.

231 Umepamba moto, uvamizi, ile saa imewadia. Naam, ndiyo, saa ya kuamua, pia, saa ya kuamua; si kuja kanisani, lakini saa ya kuamua kama utamtumikia Kristo ama utakaa vuguvugu kanisani mwako. Na hiyo ni kweli.

232 Kuna wafuasi wengi wa kanisa. Kama washirika wote... ama watu wa Marekani wanaokiri kuwa ni Wakristo, wangekuwa Wakristo halisi, Wakristo waliozaliwa mara ya pili, ndugu, tungekuwa salama tu kama vile tungalikuwa Mbinguni, ingekuwa karibu hivyo. Shida za binadamu, naam, bwana, magonjwa yangeondoka nchini, na cho chote kile.

233 Hivi lisingekuwa jambo la kupendeza kushuka kuja barabarani na kuona ambapo bibi fulani anapita, na mwanamume, "U hali gani, dada? Habari za asubuhi, ndugu"? Unashuka unaenda, hakuna...Huna hofu hata moja ulimwenguni. Kila kitu ni salama salamini. Naye huyo jamaa anakuja kwenye kona ya barabara; badala ya kujaribu kukukanyaga, angesimama, "Vema, ndugu. Vema, ilikubidi... Loo, nitangulie," mwaona, kwa hiari tu... Hivi jambo hilo lisingekuwa zuri sana? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Tutapata jambo hilo, lakini hilo ni kwenye ile Milki ya Miaka Elfu, ndugu. Hiyo siku inakuja tu. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo sasa sisi si...

234 Nilisimama kwenye ujirani wetu, hapa juzijuzi; sina kitu dhidi ya majirani wetu, lakini ninaweza kuona watoto wetu wadogo. Mke wangu alikuwa analia. Daktari fulani wa mji huu, msichana wake mdogo alikuwa anatembea na msichana wangu mdogo, nao walipendana; mpaka walipopata kujua ya kwamba jina lake ni Branham, naye alikuwa mtoto wa Kasisi Branham. Hilo lilitosha. Huyo msichana mdogo asingeweza kutembea na msichana wangu mdogo tena. "Jamani," niliwaza, "vema, sawa."

235 Baadhi ya maskini majirai walikimbilia kule, kasema, "Vema, ilikuwa sawa." Kwa hiyo, wakaenda kwa mchungaji wao. Msiniambie. Mwajua, ni—nina njia ya kujua mambo kadha, mnaona. Kwa hiyo wao—wao wakaenda kwa mchungaji wao, wakasema, "Wajua, kuna mtu fulani anayeishi karibu nasi, yeye ni mwema sana kwa wototo wetu." Kasema, "Ni Kasisi

Branham. Yeye huwachukua, anawabeba kwa gari lake ndogo la kale, na kuwachukua kwenye matembezi."

236 Kasema, "Vema," [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] "sisi hatuna neno dhidi ya Kasisi Branham. Yeye yuko sawa, lakini, mwaona, yeye ni tabaka tu ya watu tofauti na vile tulivyo sisi." Mnaona? "Sisi, ni-ningependa kwamba msinge-. . .mwajua, mimi kwa namna fulani. . .Ninyi zungumzeni nao, na mwe wazuri, lakini na liishie hapo tu."

237 Loo, ndugu! Mke wangu alikuwa amesimama pale, analia. Nikasema, "Kipenzi, ni mstari wa utengano. Mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Bwana."

238 Hata ulimwengu wote ukiangamia; bado nina Yesu Kristo! Kama itanibidi kuitwa mshupavu wa dini, kama itanibidi kuachwa na jamaa yangu, wenzangu, na vitu kama hivyo, bado nimemchagua Yesu Kristo. Ushikilie mkono wa Mungu usiobadilika. Rafiki wa duniani wakikuacha, endelea kumshikilia zaidi. Mshikilie Yeye.

239 Mungu, hebu nihuburi kuliko vile nilivyowahi kufanya hapo awali. Hebu niwahubirie watu wanaokufa, kama mtu anayekufa, mimi mwenyewe. Hebu niwahubirie watu kana kwamba sitahubiri mahubiri mengine. Hebu niwashawishi waje madhabahuni, wakiwa na nyuso zinazopiga makelele, pamoja na majonzi; warudi nyumbani na kuishi kama Wakristo, na kuishi katika ujirani wao. Wakomeshe michezo hii yote na kutangatanga, na kuruka-ruka na kupiga makelele; na kutenda namna *hii*, na kukasirikia jambo *hili*, na kwenda *kule*. Loo, msifanye jambo hilo. Huyo ni Ibilisi. Hizo roho za kipepo huwaingia Wakristo.

240 Kumbukeni, hao wahudumu huko chini, walikuwa hao manabii. Wao walikuwa manabii. Walikuwa watu wa kidini wakitoa dhabihu. Walikuwa wa kidini tu kama walivyo waalimu wa siku hizi, lakini, ndugu, walikuwa mbali sana na kujua kweli.

241 Hivi hamwoni jinsi Ibilisi alivyo wa kidini? Ibilisi si mpingaji, kitu kikubwa mno kama ukomunisti, chote kikipinga Ukristo kabisa. Sivyo ilivyo. Hayo yote ni ya Ibilisi, hakika, bali si mpinga Kristo. Mpinga Kristo ni wa kidini sana, wa kidini sana. Roho ya kidini ndiyo iliyomsulubisha Yesu. Daima imekuwa ni ulimwengu wa dini, watu wa dini, wanaosulubisha. Watu wa dini ndio waliompiga Kristo wa kweli. Manabii wa dini ndio waliompinga Mikaya. Watu wa dini leo ndio wanaoupinga Ujumbe wa Mungu.

242 Kumbukeni, nimewaonya. Nimewaambia. Mimi sana sana sizungumzi juu ya Ukatoliki, na Batisti na Methodisti; ninazungumza tu juu ya watu ambao ni watu wa utakatifu, moja kwa moja kupitia mistari hii hapa. Angalieni jambo hilo leo, jinsi limekuja na kusimama katika mchezo wa kuigiza. Loo,

jamani! Ningeingilia jambo hilo, wakati mwingine. Na moyo wangu unavunjika ndani yangu.

243 Kusimama kule na zeze ya kale, kucheza zeze hiyo ya kale, na kucheza fidla ya kale namna hiyo, "Hivi huyu ni maskini kaoboi *fulani* wa Texas?" Mimi sina neno dhidi ya huyo mtu; lakini kitu hicho ni cha kule nje ulimwenguni kule. Hiyo ni kweli. Afadhali nisimame, ndugu, bila hata kitu, na bila kitu cho chote, lakini nisimame tu na kuinua mikono yangu na kusema, "Yesu, niweke karibu na msalaba." Naam, bwana.

> Msalaba uliowekwa wakfu nitaubeba,
> Hata mauti yatakaponiweka huru,
> Kisha niende nyumbani, nikavae taji,
> Kwa maana kuna taji kwa ajili yangu.

244 Kwenu ninyi maskini mama hapa asubuhi ya leo, ambao mmekuwa mama halisi, nami ninajua kuna wengi wenu; nadhani, kila mmoja wenu. Hebu niwaambieni jambo fulani. Mungu awabariki. Ninyi ndio Injili ya tano, nafikiri. Hebu niwaambieni jambo fulani sasa kwa ajili ya watoto wenu, jambo dogo tu. Maana, Ndugu Neville labda atahubiri kwenye... juu ya mama usiku wa leo, ama ye yote yule, mmoja wetu anayehubiri, vema, juu ya mama. Lakini, sikilizeni, hebu niwaulizeni jambo fulani.

245 Kumbukeni, wakati Musa alipokuwa mvulana mdogo, mama ndiye aliyempa mawaidha. Mama mtauwa ndiye aliyemshika mtoto Musa magotini mwake, akasema, "Musa," akamfundisha kila kitu. Yeye alikuwa mwalimu wake ama...Mama alikuwa mwalimu wake, hasa, chini ya Farao, ndipo sasa akasema mambo haya. Kasema, "Musa, siku moja utawakomboa wana wa Israeli. Wewe ndiwe huyo mvulana aliyeitwa. Jiweke ukiwa msafi na asiyeharibiwa na ulimwengu, kwa maana wewe ndiwe. Wewe ndiwe."

246 Hakuna mahali pengine tunapojua, ambapo aliwahi kwenda kwenye seminari yo yote, mafundisho yo yote, aliyowahi kupata. Yeye alikaa moja kwa moja katika ikulu ya Farao, ambaye alikuwa kafiri; bali mama yake alimfundisha. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara tatu—Mh.] Huyo ndiye mama halisi. Yeye alimfundisha maagizo ya Bwana. Alimwambia jinsi anavyopaswa kuwa mtakatifu. Alimwambia ni vipi na jinsi anavyopaswa kuishi, na jinsi, yale ambayo Mungu hana budi kufanya, angemfanyia. Nayo yakadumu na Musa siku zote za maisha yake.

247 Basi mama ye yote mzuri, wa kweli, na mwaminifu atakayewachukua watoto wake wachanga, badala ya kuwatuma kwenye sinema na dansi, na kadhalika namna hiyo, naye atawapakata pajani mwake na kuwafundisha habari za Bwana Yesu Kristo!

248 Hapa hivi majuzi, nilikuwa nikizungumza na mama fulani kwenye simu. Ndipo huyo mama akasema, "Loo, Ndugu Billy," akasema, "maskini mvulana wangu yuko katika shida." Kasema, "Loo, jinsi alivyo katika shida!"

249 Nikasema, "Naam, najua habari hizo, dada, mpenzi." Naye akasema, "Huenda amekosea. Sijui mimi." Kasema, "Mtu mmoja anasema *hivi* na mwingine anasema *vile*. Sijui. Lakini," kasema, "haidhuru kama amekosea ama hajakosea, mimi nampenda." Naam, basi, "Ninampenda."

250 Yeye akamwambia mamaye, kasema, "Nimedanganywa sana na *hiki* na *kile*." Kasema, "Mama, ninaamini wewe ndiye mpenzi pekee niliye naye kweli; mwanamke aliye mwaminifu kwangu, wala haniachi." Huo ni upendo wa mama. Huyo ni mama halisi atakayemkumbatia mtoto wake mchanga. Haidhuru kama hajakosea ama amekosea, yeye anamwendea moja kwa moja. Na iwapo Mungu... Kama mama anaweza kuwazia jambo hilo juu ya mtoto wake mchanga, ni zaidi sana vipi Mungu atawazia juu ya walio Wake! Mnaona? Ninyi dumuni moja kwa moja pamoja Naye. Enendeni vizuri.

251 Basi sasa hebu niwaambieni tu mama mwingine, upesi sana, katika Biblia, kabla hatujafunga. Kulikuweko na mama jina lake Herodia. Alimfundisha bintiye dansi ya kurukaruka. Alitaka yeye apendwe na watu wengi. Ndipo akacheza mbele ya mfalme, kisha akataka kichwa cha Yohana Mbatizaji. Tuna rekodi ya watu sabini wa ukoo wake, msichana huyu aliyecheza mbele ya... Binti ya Herodia alicheza mbele ya Herode; watu sabini wa ukoo wake, aidha walikufa wakiwa malaya ama walinyongwa.

252 Mama mmoja alimfundisha bintiye mambo ya ulimwengu; huyo mama mwingine akamfudisha mwanawe mambo ya Mungu. Mmoja akawa kiongozi mkuu na mshindi, anayekumbukwa daima kati ya wanadamu siku hizi; na huyo mwingine anateseka na yuko kuzimu, na amewachukua maelfu mara maelfu pamoja naye. Mnaona ninalomaanisha? "Mlee mtoto kwa njia impasayo."

253 Nami kweli nawahurumia ninyi maskini akina mama mlioketi hapa huku mmevaa waridi zenu nyeupe. Kuna Mbingu ambayo mama fulani ameenda, leo, ambako mama mwema wa mtindo wa kale aliyemwishia Mungu, labda amepita ng'ambo ya pazia. Anakungojea uje. Hiyo ni kweli.

254 Ninawaheshimu na kuwastahi ninyi hapo mlio na waridi zenu nyekundu. Mama yenu, kama mkitaka kumfanyia jambo lo lote, fanyeni hivyo siku mia tatu na sitini na tano za mwaka. Nendeni nyumbani mwake mkaombe, na mkamwishie Mungu. Hilo ndilo jambo la kufanya. Kisha mkawalee watoto wenu. Na wakati watoto wenu watakapokua, watawaita "wabarikiwa," baada ya ninyi kuvuka ng'ambo ya pazia. Hiyo ndiyo roho halisi

ya umama, roho halisi ya sikukuu ya mama. Sikukuu ya mama ni siku mia tatu na sitini na tano za mwaka.

255 Hii ni siku wanayouza maua na kutoa zawadi. Ulimwengu unafanya jambo hilo. Kama ukipita, kama ulimwengu ukidumu miaka mingine ishirini, wao watakuwa na sikukuu za mwana, na sikukuu za binti, na, ama sikukuu za binamu, na sikukuu za mjomba, na mambo hayo yote namna hiyo, ya kutosha tu kuutia ulimwengu katika viinimacho vya kibiashara. Huko ndiko tu unakoelekea, moja kwa moja kuzimuni, upesi uwezavyo kwenda, kwenye uharibifu.

Lakini, ninyi, Mungu awabariki, ndilo ombi langu. Na tuombeni.

256 Baba yetu mwema wa Mbinguni, tunapoangalia nyuma, asubuhi ya leo, na nia zetu, kule nyuma, miaka mia kadha iliyopita, wakati aliposimama Yehoshafati pale karibu na Mfalme Ahabu. Nayo ile roho ndogo ndani ya moyo wake, iliyosalia ya Mungu, ingawa alikuwa amefanya kosa, ilimwambia, "Hili ni kosa. Hili ni kosa. Si safi. Si takatifu. Nabii amesema mambo haya yasingeweza kuendelea namna hii." Nao ule Moto mdogo wa Mungu ukamwamsha.

257 Halafu ulikuwa na mtu fulani wa kujibu huo Moto mdogo, ambaye alikuwa ni Mikaya, nabii wa kweli wa Mungu. Ingawa huenda alikuja kule amevalia matambara, ingawa huenda alikuja kule akiwa anachukiwa, na wote hao wakimwangalia kama kundi la mbwa mwitu likimwangalia mwana-kondoo. Bali alisema kweli, ingawa ilimbidi kupigwa kofi la usoni, ingawa ilimbidi kutupwa gerezani na kulishwa mkate na maji ya hofu. Lakini, hata hivyo, maneno aliyosema yalitimia, kwa maana Wewe ulikuwa pamoja naye.

258 Mungu, jalia, leo, nasi tunaangalia kwenye Biblia hii. Tunaangalia kwenye vitabu vya kanisa, zile amri kumi, na kadhalika, za makanisa, zile taratibu, na kuona jinsi wanavyofanya jambo *hili*, *lile*, ama lile *lingine*. Lakini hebu na tuangalie katika Neno hili la kweli hapa, tuone lilivyosema. "Bila utakatifu, hakuna mtu atakayemwona Bwana. Ifuateni amani na utakatifu, ambao, bila huo, hakuna mtu atakayemwona Bwana. Yeye aipendaye dunia, wala mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hakumo ndani yake."

259 "Katika siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kujisifu, wenye kiburi." Loo, mambo hayo makubwa, Bwana, yanayotukia! "Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wakiwafundisha watu kanuni za—za wanadamu badala ya maagizo ya Mungu; wenye mfano wa utauwa, huku wanakana Nguvu za Roho Mtakatifu" kumfanya mtu ajazwe na Roho, kumfanya afurahi, kuyafanya machozi yatiririke machoni mwake, kumfanya atoke aende akawaombee

wagonjwa, kumfanya anene kwa lugha na kufasiri, kumfanya atoe unabii. Roho wa Mungu, Mungu aliye hai, walimchukua tu wakamwingiza Yeye kwenye nyumba fulani ya kulala ama kitu kama hicho, "Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake."

260 Ee Mungu, jalia kusayiko hili dogo, leo hii, waamke upesi, sasa hivi, kabla ya wakati wa mwisho, wakashikwe katika hali hii. Jalia kwamba sisi tuwe, tukijifanya upya, kama ilivyosema Biblia, "Amkeni mkajitikise. Mkaulize juu ya ile njia ya kale, ambayo ndiyo njia njema; na mtakapoipata, mkatembee ndani yake." Mungu, jalia kwamba tuweze kuiona ile njia ya kale iliyoparuza, ambapo tunaweza kusimama pamoja tena, kama mamia, na kushikana mikono na kuimba.

> Nitashika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa.
> Nimeanza na Yesu, nami nitafaulu.
> Mungu, tusaidie tuishi namna hiyo na tuwe hivyo!

261 Wabariki hawa mama wote wapendwa walioketi hapa, Bwana; wakijua ya kwamba wao ni mama, wao wenyewe, huku waridi nyekundu zimefungiliwa kwenye makoti yao, asubuhi ya leo, kama kumbukumbu ya maskini mama mpendwa ambaye amevuka ng'ambo ya pili. Ee Bwana wa Uzima, wabariki, Bwana. Na wao wabarikiwe, pia, na kumbukumbu la watoto wao liwe kama lao lilivyo juu ya mama yao, kama amekwisha kwenda ng'ambo ya pazia, kwenye Mbingu yenye utukufu. Jalia jambo hilo, Bwana.

262 Na asubuhi fulani wakati maisha yanazifunga vena zetu, na pumzi yetu inashindwa kuja kwetu, ile pazia itafunguka; yeye atashuka, labda, kwenye mwisho wa Yordani, kutusaidia kuvuka. Loo, kwenye hiyo siku yenye fahari tutakapokanyaga kwa miguu yetu huko ng'ambo, ambako hakutakuwa . . . Hewa haitakuwa imechafuliwa na moshi wa sigara. Hakutakuwako na mlevi barabarani. Hakutakuwako na malaya. Hakutakuwako na dhambi kamwe. Hakutakuwa na kitu kama hicho. Lakini, katika ile milele yenye utukufu, tutaishi kwa amani na Bwana wetu Yesu Kristo pamoja na watoto wetu. Na, loo, ni siku ya ajabu namna gani!

263 Ee Baba, wakati lile giza kuu linaendelea, vile vita, huku Ibilisi anazivamia nchi, na kuivamia mimbara, kuyavamia makanisa, kuwavamia watu, kuzivamia biashara, kuivamia miji, na shule na nyumba; Ee Mungu, tusaidie kusimama, tuuvute upanga upesi na tukampiganie Mungu, kama vile Musa na wale—na wale Walawi walivyofanya kule chini wakati dhambi ilipokuwa kambini. Tusaidie, Bwana.

264 Tusamehe sasa, na utubariki. Na utuweke tukiwa wanyenyekevu, tupondeponde, Bwana. Ee Mungu, Wewe

ulisema, "Yeye anayekwenda, akipanda katika machozi, bila shaka atarudi tena, akifurahi, akileta miganda." Ee Mungu, tuvunje vipande-vipande. Tufinyange, upya, Bwana. Tunatoka njiani sana.

265 Mimi, mwenyewe, Bwana, ninafikia mahali ambapo ninafikiri juu ya ni wangapi watakaohudhuria mkutano wangu. Ee Mungu, ninakutaka Wewe uhudhurie. Njoo, Bwana! Ee Kristo, njoo Bwana! Nipondeponde; nifinyange. Ee Bwana, usi-, usiniruhusu kamwe kuweka mambo hayo niani mwangu. Mungu, yaweke mbali nami!

266 Nisaidie, Bwana, kuhubiri, kama nilivyosema, muda kidogo uliopita, kama mtu anayekufa kwa watu wanaokufa, tukijua ya kwamba sisi sote hatuna budi kuukabili Umilele. Hatuna budi kusimama mbele Zako; wakati Wewe hauko katika hali yako ya kupendeza, wakati Wewe huna huruma; wakati Wewe umesimama bila rehema; wakati Wewe umesimama, mwenye hasira, kuleta hukumu juu ya mataifa na watu ambao wameukataa na kuupuuza upendo wa Mtoto Wako.

267 Mungu, nipe rehema pamoja Naye leo, ili kwamba katika Siku ile niweze kusimama nimehakikishiwa. Huenda ikanibidi kulia sasa, lakini Wewe utayafutilia mbali, tupate furaha, wakati ule, utakaposema, "Ingieni katika furaha ya Bwana, iliyoandaliwa kwa ajili yenu tangu kuwekwa misingi ya dunia." Mungu, uwe pamoja nasi sasa, ukatusaidie, tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Kuvamiwa Kwa Marekani SWA54-0509
(The Invasion Of The United States)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, 9 Mei, 1954, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1994 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1994 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org